# Nipashe

Jumatatu Aprili 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581661

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**ACT** Wazalendo walia maoni ya wadau kukaliwa

UKURASA 4



**Waandishi** wakumbushwa kuzingatia amani kuelekea uchaguzi

UKURASA 5



**Watoto** sita wafariki, watatu wa familia moja kwa kudondokewa na nyumba

UKU. 7


**NYOTA WANAOWANIA KIATU CHA DHAHABU ULAYA 2023-24**

UKURASA 12-13

# Hofu chanjo saratani mlango wa kizazi

• **Wataalamu** waeleza matokeo ya... *Uk. 2*





Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha,amezindua rasmi kampeni ya utoaji chanjo ya saratani ya mlango wa shingo ya kizazi (HPV) kwa wasichana huku akitoa onyo kwa atakaye bainika kufanya upotoshaji kuhusu chanjo hiyo Serikali itamchukulia hatua. **PICHA: MAKTABA**

UKURASA WA 7

## ADAIWA KUMUUA RAFIKI YAKE KWA KISU WAKICHEZA MUZIKI



MKAZI wa Tegeta jijini Dar es Salaam, Kadi Msela, ameuawa kwa madai ya kuchomwa kisu na rafiki yake aliyetajwa kwa jina moja la Amir, wakati wakicheza muziki baa...

## Rais wa Somalia aenda kujifunza MOI, JKCI

UKURASA 3



## Lissu: Waliotajwa Ripoti ya CAG wawajibishwe

UKURASA 3

**MICHEZO** **BENCHIKHA ATOA SABABU KUVUNJA MKATABA** UK.24 **MAONI,** UK.6



Chanjo ya saratani

# Hofu chanjo saratani mlango kizazi

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAM wa afya nchini wamewatoa hofu wananchi usalama wa chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka tisa hadi 14.

Tangu kuanza kutolewa kwa chanjo hiyo, kumekuwa na hofu kwa jamii hasa wazazi kuhusu usalama, huku baadhi wakiwazuia watoto wao kuchanja wakiamini zimeletwa kupunguza uwezo wa Watanzania kuzaa.

Maswali ni kuhusu umri wa watoto wanaopatiwa chanjo hiyo wa chini ya miaka 14 ilhali madhara huonekana kuanzia miaka 24.

Aidha, watoto wa kiume kutopatiwa chanjo hiyo na dozi kuwa moja badala ya tatu kama awali, huku wanaoshi na VVU kupata dozi tatu tofauti na wengine.

Vile vile, muda wa chanjo kuimarisha kinga ya mtumiaji na kama ni hiyari na madhara kwa asiyepatiwa chanjo hiyo.

Jopo la madaktari na watafiti wabobezi katika afya ya uzazi walifanya mjadala ulioendeshwa na jukwaa la Jamii Forum kupitia mtandao wa kijamii wa X, na kueleza kuwa kuna umuhimu wa chanjo hiyo kwa kundi lengwa la watoto.

Akizungumzia usalama wa chanjo hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Wizara ya Afya, Dk. Ntuli Kapologwe, aliwatoa hofu Watanzania kuwa tangu ianze kutolewa mwaka 2014 kwa wakazi wa Kilimanjaro hawajapata taarifa ya mtumiaji kupata madhara yoyote.

Alisema utoaji wa chanjo hizo katika awamu ya kwanza uliendа sambamba na ufuatiliaji wa karibu, ili kuchunguza kama kuna madhara yoyote makubwa yanayoweza kujitokeza na kuyafanyia kazi, lakini hakukuwa na taarifa yoyote.

Alisema baada ya kujiridhisha na usalama wake waliendelea kutoa chanjo hiyo na mwaka 2018 waliizindua rasmi, na kuendelea kuitoa kwa dozi ya mara mbili kila baada ya miezi sita, lakini mwaka huu wamebadili na kutoa moja baada ya utafiti kuonyesha zote zinafanya kazi sawa.

Alisema serikali imetilia mkazo kutolewa kwa chanjo hiyo kwa sababu saratani ya mlango wa kizazi ndio inayoongoza kuathiri watu kwa asilimia 23 kati ya aina zote za saratani zilizopo nchini, ikifuatiwa na saratani ya mfumo wa chakula na matiti.

"Gharama ya matibabu ya saratani hususani ya mlango wa kizazi, serikali imefanya uchambuzi na kuona kwamba mtu anayekwenda kwa matibabu ya saratani hiyo ina mgharimu zaidi ya Shilingi milioni nane kwa kuanzia na zaidi kutegemea na ukubwa wa ugonjwa," alisema.

Akijibu swali la mshiriki aliyetaka kufahamu kama chanjo hiyo ina uwezo wa kuzuia mwanamke kubeba ujauzito, Daktari Mkufunzi kutoka Wizara ya Afya, Norman Jonas, alisema kuwa hakuna uhusiano wowote wa chanjo hiyo na mtu kutobeba ujauzito.

"Tafiti za kisanyansi zinaonesha umri sahihi wa kutoa chanjo ni miaka tisa hadi 14 ikiaminika ni umri ambao ni kabla ya balehe. Virusi vya HPV vinaathiri binadamu, na maambukizi yake yanapotokea hayana dalili," alisema.

Alisema virusi vya saratani ya mlango wa kizazi (HPV) vinaathiri watu wengi na havina dalili, kati ya watu 100 waliopata maambukizi ya ugonjwa huo, 90 yawametokana na virusi hivyo vilivyopo vya aina 200, huku asilimia 40 ya maambukizi yakipatikana kupitia kushiriki ngono.

Akijibu swali la mdau aliyetaka kufahamu kwa nini chanjo hiyo inatolewa kwa mabinti wa umri wa miaka tisa hadi 14 ilhali watu walio hatarini kupata maambukizi ni kuanzia miaka 25, Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo Dk. Florian Tinuga, alisema hutolewa kwa watoto wa umri huo kwa kuzingatia utafiti wa kisayansi.

Alisema chanjo hiyo ni hiyari, lakini anashauri watoto wapatiwe kwa sababu ni muhimu na salama kwa mabinti hao, na inatolewa bure katika vituo vya afya na hospitali za serikali na binafsi pamoja na kuwafuata watoto hao katika shule wanazosoma.

Alisema katika kundi hilo chanjo ya dozi tatu itatolewa kwa mabinti wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na wasioishi na virusi hivyo watapatiwa dozi moja.

Alisema hadi kufikia Aprili 26, mwaka huu ugawaji wa chanjo ya dozi moja ya HPV uliwafikia karibu asilimia 90 ya walengwa tangu kuanza kutolewa Aprili 22, mwaka huu hali inayoonyesha kuna hamasa kubwa katika jamii.

**WENYE VVU**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mataalam wa Magonjwa ya Jamii, Dk. Maryam Amour, aliwashauri wenye VVU kufanya uchunguzi wa saratani hiyo wakiwa na umri wa kuanzia miaka 25 kwa kuwa wapo hatarini zaidi kupata maambukizi.

Alitaja kundi lingine lililo hatarini ni wanawake walio katika umri wa miaka 30 hadi 50 na kuwashauri kufanya uchunguzi kila baada ya miaka mitatu, ili wanapobainika waanze tiba mapema kabla ugonjwa haujawa mkubwa na kushindwa kutibika.

Alisema utatifi uliofanyika katika nchi tisa ikiwamo Tanzania ulionesha wasichana wengi wanaanza kujamiiana wakifikisha umri wa miaka 15 na kuendelea, ndio maana hata chanjo hiyo imeanza kwa wasichana wenye umri wa miaka tisa hadi 14 ili kuwaepusha kupata maambukizi wakiwa na umri mdogo.

**Jopo la madaktari na watafiti wabobezi katika afya ya uzazi walifanya mjadala ulioendeshwa na jukwaa la Jamii Forum kupitia mtandao wa kijamii wa X, na kueleza kuwa kuna umuhimu wa chanjo hiyo kwa kundi lengwa la watoto.**

Dk. Maryam alisema nchi zilizoanza kutoa chanjo hizo kwa muda mrefu na kuchanja zaidi ya asilimia 90 ya walengwa ikiwamo Australia wamefanikiwa kupunguza matukio yote yanayotokana na maambukizi ya kirusi cha HVP.

"Australia pamoja nchi nyingine 40 zinatoa dozi moja ya chanjo hiyo kama ilivyo Tanzania na ukiangalia kwenye takwimu Australia ndio nchi yenye kesi chache za kansa ya mlango wa kizazi ulimwenguni na kufikia malengo ya dunia," alisema.

Alisema Tanzania kwa sasa wanachanja watoto wa kike pekee kutokana na uwezo, lakini tatizo hilo linawapata na wanaume.

**.WAZAZI WANENA**

Mmoja wa wazazi walioshiriki mjadala huo, Happy Enea, alisema amejifunza na kupata uelewa mpana kuhusu chanjo hiyo kupitia kwa madaktari hao na atamruhusu mtoto wake apatiwe chanjo hiyo shuleni au kumpeleka kwenye kituo.

Kabla ya kupata elimu hiyo alimkataza mwanawe kupata chanjo hiyo akiamini itamletea madhara ikiwamo kutobeba ujauzito kutokana na maneno aliyokuwa akiyasikia kwa watu.

"Akiwa shule ya msingi walimu walinipigia simu mara mbili kunishauri mwanangu apatiwe hiyo chanjo nikakataa, juzi pia akiwa sekondari walimu wake walinipigia simu nikakataa, lakini jana nikasema kwa nini nisiingie kwenye huu mjadala nisikie mwenyewe kama kweli kuna madhara, kumbe hakuna ni salama," alisema Happy.

Aidha, aliishauri serikali kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa jamii ikiwezekana elimu hiyo itolewe hospitali kwa wagonjwa wanaokwenda kila siku, vituo vya mabasi, ofisini na hata kuweka matangazo kwenye luninga ili elimu iwafikie watu wengi zaidi kwa kuwa sio kila mtu ana uwezo wa kusikiliza mijadala ya mitandaoni.

# Rais Somalia aenda kujifunza MOI, JKCI

**Na Halfani Chusi**

RAIS wa Jamhuri ya Somalia Hassan Mohamud, ametembelea taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwaajili ya kujifunza namna zinavyofanya kazi ya kuokoa maisha ya watu.

Alitembelea taasisi hizo baada ya kufanya mazungumzo mafupi na Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu.

Aliambatana na Waziri wa Afya nchini humo na wafanyakazi wengine kwa lengo la kujifunza.

Akizungumzia ugeni huo, Waziri wa Afya nchini, Ummy Mwalimu, alisema marais hao walijadiliana maeneo matatu ya ushirikiano ikiwamo kutoa huduma za matibabu ya kibingwa na ubobezi.

Aliyataja maeneo mengine waliyokubaliana kushirikiana ni katika mafunzo ya wataalamu wa afya na usambazaji wa dawa kupitia Bohari ya Dawa (MSD).

"Nchi yetu imefanya vizuri kuboresha huduma za kibingwa JKCI na MOI tumemweleza Rais wa Somalia kwamba tupo vizuri, tuna vifaa tiba vya kisasa na tuna madaktari bingwa bobezi ambao wamejengewa uwezo na uzoefu mkubwa.

"Na wao tumebaini elimu yao inaishia ngazi ya shahada ya kwanza tutashirikiana nao kutoa mafunzo ya ubingwa katika vituo vyetu vya afya hasa kupitia hiki cha Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

"Bohari yetu ya dawa imekuwa na uzoefu mkubwa, tunahudumia zaidi ya vituo 4,000 nchini Mawaziri wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wameipa dhamana kununua dawa kwaajili ya nchi za jirani kwa kuzingatia ubora na urahisi wa bei," alisema Waziri Ummy.

Alisema kinachofuatia atakaa na Waziri wa Afya wa Somalia kujadiliana lini waanze kutekeleza malengo makubwa yaliyowekwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Prof. Abeli Makubi alisema lengo la ziara ya Rais huyo ni kuongeza ushirikiano katika tiba utalii na wameshawishika kuja kutokana na ubora wa huduma wanazotoa na uwezo wataalamu waliopo.

Alisema wamemwahidi kutoa ushirikiano wa matibabu kwa watu wa Somalia na kuwajengea uwezo katika eneo la tiba ya mifupa na ubongo.

"Ujio wake unaifanya MOI kukuza jina kimataifa na kuongezeka kwa kipato kupitia wagonjwa watakaokuja kutibiwa kutoka nchini kwao.

"Kule Somali baadhi ya wananchi huwa wanapata ajali kwahiyo tukiwapa huo ujuzi, tunaweza tukawasaidia kwa kuwauzia vifaa vya upasuaji kwa sababu vipo vinavyokuja hapa tunaweza kuangalia namna ya wao kuchangia kidogo," alisema Makubi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema ugeni huo umekuja baada ya mafanikio makubwa waliyopata tangu taasisi hiyo ilipoanzishwa mwaka 2015.

Alisema kwa sasa imekuwa miongoni mwa taasisi kubwa Afrika na ya kwanza Afrika Mashariki kwa matibabu ya moyo.

"Amekuja kujionea huduma zinazotolewa katika taasisi yetu, na vilevile ataenda kuleta wananchi wake kutibiwa hapa kwa sababu kutoka huko kuja hapa ni karibu tofauti na nchi za Ulaya," alisema Kisenge na kuongeza;

Kuhusu ongezeko la wagonjwa kutoka nje kama wataielemea taasisi, alisema wamejipanga vyema na serikali imetoa Hospitali ya Dar Group na kuna jengo litaanza kujengwa eneo la Mikocheni.

Pia alisema Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wanaimarisha vyumba vya daraja la juu (VIP), tutakuwa na tawi Masaki na Kawe, na kwamba kuna uimarishwaji wa tekonolojia kiasi cha mtu kutibiwa akiwa nyumbani.

# Lissu: Waliotajwa Ripoti CAG wawajibishwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA



MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Tundu Lissu, amesema ripoti inayotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kila mwaka wanaotajwa kuhusika na ufisadi hawachukuliwi hatua kwa sababu wahusika ni baadhi ya viongozi.

Akihutubia mamia ya wananchi mjini Singida mwishoni mwa wiki baada ya kushiriki maandamano ya chama hicho yanayoendelea katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kushinikiza Katiba mpya, mabadiliko ya kikokotoo na kuchukua hatau kunusuru hali ngumu ya maisha, alisema kila mwaka ripoti ya CAG inaeleza wizi, lakini wahusika hawachukuliwi hatua.

"Kila mwaka tangu nijue kusoma na kuandika sijawahi kuona CAG akitoa ripoti kwamba mwaka huu mahesabu yameenda vizuri, kila mwaka ni orodha ya wizi wa pesa za wananchi, Rais anajua, mawaziri wake wanajua, wakuu wa mikoa wanajua, wote wanajua kwanini hawachukui hatua, unafikiri ni kwanini kama sio wao ndio wahusika," alisema.

Lissu alisema suala la tozo, kikokotoo na kodi ni biashara ya baadhi ya viongozi na ndio maana mambo hayo hata wananchi na watumishi wakipiga kelele hawasikilizwi.

Alisema ili kuondokana na mambo hayo ndio maana CHADEMA imeamua kuanzisha maandamano nchi nzima kudai Katiba mpya ambayo itakuwa ni suluhisho la mambo yote na wananchi kupata haki zao.

"Tunaandamana sababu tumechoka na tusipoandamana CCM hii itatuangamiza si wananchi wa vijijini, mijini pekee yao, lakini ni pamoja na watumishi wa serikali sababu na wao wamechoka, mfano suala la kikokotoo askari, wauguzi, mabwana shamba na watumishi wote kwa ujumla kinawaumiza," alisema.

Akizungumzia wafanyabiashara wawili wa Mkoa wa Singida ambao ndugu waliotekwa tangu mwaka jana akiwataja kwa majina, alisema ana taarifa kuwa baada ya kutekwa walipelekwa katika Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

"Ndugu wa wafanyabiashara hawa wamekwenda polisi na katika vyombo mbalimbali vya serikali, lakini hawajapata msaada wowote, hivi hawa watu wanaoitwa wasiojulikana wanatoka wapi, kwanini hawa polisi wanapata kigugumizi hawataki hii taarifa kama sio kwamba wametekwa na watu wa serikali," alihoji.

Kuhusu Soko la Kimataifa la Vitunguu Misuna lililopo katika Manispaa ya Singida, alisema ni aibu kulipa soko hilo jina hilo wakati ukweli halina hadhi hiyo na kuna uchafu.

"Tumepita soko la kimataifa la vitunguu, kimsingi tusiwaambie watu kwamba tuna soko la kimataifa hilo sio soko halistahili hata kuwa soko la mtaa, kata wala manispaa na kama mnaita lile ndio soko la kimataifa basi mkoa huu wa Singida hakuna anayejua masoko yenye hadhi ya kimataifa," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sera Kanda ya Kati, David Djumbe, alisema CHADEMA inafanya maandamano kwa sababu wananchi wamechoka kuibiwa kwenye uchaguzi unaofanyika na kuongozwa na watu wasiozijua shida za wananchi.

"Watu walioshiba huwa hawaandamani, wanaopata huduma nzuri huwa hawaandamani, tunaandamana sababu miaka 60 ya Uhuru na Muungano Serikali ya CCM bado haijatatua kero za wananchi," alisema Djombe.

Wakili wa kujitegemea, Boniface Mwambukusi, alisema wananchi wanataka Katiba mpya itakayoleta uwajibikaji ili kila kiongozi anayefanya mambo ya ovyo achukuliwe hatua.

"Katiba ndio sera na msingi wa mambo yote ya nchi, tunataka Katiba itakayolinda haki za watu na sio hivi sasa ambapo watu wanatekwa na kupotezwa kusikojulikana, tunakata katibu bora ili kuleta mgawanyiko sawia kuwa na Bunge lenye msimamo, sasa hivi tuna bunge ambalo ni bovu na bora livunje," alisema.

Akizungumza katika ibada ya kuliombea taifa, mapema wiki iliyopita, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema serikali imeelekeza mawaziri kuhakikisha hoja za CAG zinajibiwa na hatua madhubuti kuchukuliwa.






Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) Dk Adelhem Meru (wapili kushoto) akiangalia vifaa vya uokoaji alipotembea banda la Barrick jana kwenye maonesho ya OSHA yanayoendelea katika viwanja vya Nane Nane mjini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT Wazalendo yalia maoni kukaliwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUTANO Mkuu wa Kidemokrasia wa Chama cha ACT Wazalendo, umeibua hoja ikiwamo madai kuwa kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia Zanzibar yamekaliwa, hayajafanyiwa kazi, huku hoja kuhusu Zanzibar yenye mamlaka kamili ikitawala.

Aidha, madai ya kuwapo viashiria hali ya nchi kiuchumi kutokuwa nzuri.

Kiongozi mpya wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, akizungumza katika maadhimisho ya miaka 10 ya kuzaliwa chama hicho na mkutano wa kidemokrasia uliofanyika Moshi, Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, alisema miaka 10 ya ACT Wazalendo imekuwa ikipitia kwenye pumzi ya moto.

Alisema kwa sasa mabega yake ni mazito na chama chake kinaona sera zinazotekelezwa na Serikali ya CCM hazijali maslahi ya wengi, badala yake viongozi wa kisiasa na umma wanatumia mwanya kujiimarisha katika maslahi binafsi dhidi ya umma na kuzima ndoto za ujenzi wa taifa la watu wote.

Aidha, Chama hicho kimetangaza rasmi Mei 5, mwaka huu, kuanza kutumia nembo yake mpya na bendera mpya, kujipanga kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji wa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025.

"Pamoja na kwamba nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi, raia wake kwa umoja wao hawafaidiki na rasilimali, lakini zinaendelea kuwaneemesha watu wachache walio serikalini, mashirika ya umma na kampuni za kimataifa.

"Bado, uchumi wa taifa huru unaendelea kuwatajirisha watu wa nje na wachache wa ndani ya nchi, huku mamilioni ya Watanzania wakifukarishwa."

Semu, ameeleza kuwa Watanzania wanaweza kuona viashiria kadhaa vya hali ya nchi yao kiuchumi sio nzuri na haielekei pazuri, akieleza kasi kubwa ya ukuaji wa deni la serikali, kutishia maendeleo ya watu, uwezo wa nchi kujihudumia na kusababisha ukuaji wa uchumi unaoendeshwa na deni (debt driven growth).

Suala la huduma za afya na kupaa kwa gharama za matibabu, kukosekana kwa huduma bora au kutokuwapo kwa miundombinu itakayowaweza wananchi kuyapata.

Aidha, akizungumzia ukosefu wa ajira na kipato cha uhakika, alisema kuwa takwimu zinaonyesha vijana milioni moja wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka, ni 67,000 pekee wanaoweza kuajiriwa.

"Kwa hiyo, nguvu kazi kubwa iliyotupwa nje ya mfumo wa uzalishaji inatumika kuwanufaisha watu wachache kwa kuzalisha faida zaidi, huku wakiwafukarisha na kuwadunisha mamilioni ya Watanzania, alieleza katika hotuba yake.

Kwa ufupi, hoja nyingi zinazotolewa hazididisi kiini cha tatizo la ukosefu wa ajira nchini kwetu."

Kuhusu kikokotoo cha mafao kwa wastaafu alisema, matumizi ya kanuni mpya za kikokotoo kwa kumlipa mstaafu asilimia 33 ya mafao ya mkupuo kwa miaka 12.5 na kikotoo cha 1/580 ni kuwakandamiza na kuwanyonya wazee waliotumikia taifa katika mazingira magumu ya mishahara ya chini inayowafanya kuishi kwenye mzunguko wa madeni.

Semu, alisema kanuni hizo zinashusha ari, hamasa na ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi.

Kuhusu hali ngumu ya maisha na umaskini, alisema kwa picha ya jumla, hali ya kiuchumi inawaonyesha kuwa bado mapambano yao ya kuhakikisha rasilimali za nchi zinatumika na zinalinufaisha taifa (kwa maslahi ya wote na sio wachache wale wale), yanapaswa kuendelea na kuongezewa nguvu.

Makamu Mwenyekiti Bara na Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, wakati wa mjadala wa mwenendo wa demokrasia nchini kuelekea chaguzi zijazo, alisema chama hicho hakiko tayari kushuhudia hujuma za uchaguzi na waliowahujumu waje mbele yao wameinamisha shingo.

Kuhusu Sheria za Uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi, Mchinjita, alisema hawana tatizo la maoni yaliyotolewa na Kikosi Kazi cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa yapo na yamewekwa hadharani na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Samia Suluhu Hassan).

Hata hivyo, alisema shida yao ni maoni ya Kikosi Kazi cha Zanzibar, kushikiliwa bila kufanyiwa kazi.

Zitto: Natamani ningefanya biashara

Mwasisi na Kiongozi wa zamani wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe akichagiza mjadala kuhusu mwanzo mpya wa chama hicho, operesheni ya shusha tanga alisema:

"Nadhani jambo ambalo ningepaswa kulifanya kama maisha yangu yangerudi tena nyuma miaka 20 ni kufanya biashara. Mimi nilikuwa siamini kabisa kwamba ukiwa kiongozi hupaswi kufanya biashara, nilikuwa naamini hivyo hata kuuza maandazi; kwa sababu utafanya maamuzi yenye mgongano wa maslahi na imekuwa hivyo muda mrefu.

"Lakini mara baada ya kuwa kiongozi wa ACT Wazalendo, sasa moja kati ya kazi ya viongozi wa chama yeyote duniani kote; kazi yake ya kwanza ni fund raising between 65 and 75 percent (kutafuta fedha kati ya asilimia 65 mpaka 75) ya muda wa viongozi wa chama. Kwa hiyo mkimsikia Doroth (Semu) anasema mabega mazito ni kwa sababu hiyo.

Miaka 10 ya uongozi wangu, nimejifunza nilikosea sana kuacha kufanya biashara. Kwa sababu katika kazi za chama mfano shughuli kama hii inahitaji gharama za usafiri, wafanye nini, halafu chama hakizalishi, pesa za chama unaziomba kwa watu.

Unaishi kwa kugongea wafanyabiashara. Anajua tu huna, lakini anakwambia atakupa halafu mpaka kesho shughuli anakuambia mambo yangu yameenda vibaya bwana!

## Watu milioni nne Afrika wafa kila mwaka kisa nishati chafu

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk.Selemeni Jafo amesema takwimu zinaonesha watu milioni nne Afrika wanapoteza maisha kila mwaka kwasababu ya kutumia nishati chafu ikiwemo ya kuni na mkaa.

Hivyo, amesema ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuanzisha kampeni ya kuhamasisha nishati safi Afrika inapaswa kuungwa mkono na watu wote.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya kukabidhi mitungi ya gesi 1,500 na majiko kwa wananchi wa Jiji la Arusha wakiwemo wajasiriamali.

Dk. Jafo alisema matumizi ya kuni na mkaa nchini yanasababisha hekta 46,242 za miti kupotea kila mwaka kwasababu wananchi wanakata kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

Dk.Jafo alisema matumizi ya nishati safi inakwenda kuunga mkono juhudi za Rais Samia katika kampeni ya kuhamasisha nishati safi.

"Rais Dk.Samia Suluhu Hassan amekuwa na dhamira njema na ndiyo maana amekuja na kampeni ya nishati safi ya kupikia. Haya ni mapenzi yake na kwasababu tunafahamu nishati chafu inamadhara makubwa katika mazingira," alisema Jafo.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa kinamama na wasichana kwa asilimia kubwa wanatumia wastani wa saa 20 kwa wiki kwa ajili ya kutafuta kuni na mkaa.

"Leo hii ukiona nchi imejipanga katika nishati safi ya kupikia ni jambo la msingi lenye kutia matumaini. Watafiti wanatuambia kitendo cha kutumia nishati safi ya kupikia kwa akina mama wajazito kunasaidia kurekebisha presha ya mama mjazito," alisema Dk. Jafo.

Alisema nishati safi inasaidia mama mjazito kupata mtoto mwenye uzito unaokubalika anapozaliwa, hivyo kuna faida nyingi kutumia nishati safi ya kupikia.

"Nina fahamu mpaka leo hii Oryx wameshatoa mitungi ya gesi 32,000 kwa ajili ya jamii na wameshatumia Sh.bilioni 2.7 lakini bado wameendelea kuendelea na kampeni hiyo kwa kutoa mitungi kwa jamii," alisema Dk. Jafo.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo alisema katika kuunga mkono jitihada za Rais Samia kuhamasisha nishati safi ya kupikia wameona ni vema kuendelea kuyagusa makundi mbalimbali katika jimbo hilo.

Alisema kabla ya kugawa mitungi hiyo 1,500 ya Oryx kwa wakazi wa Arusha Mjini, tayari ameshagawa pia mitungi 1,400 kwa wajasiriamali, huku akisisitiza wataendelea na kuyafikia makundi yote yakiwemo ya watoto wanaolelewa vituo vya ya watoto yatima.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya gesi ya Oryx, Benoite Araman alisema Tanzania, wananchi 33,000 wanapoteza maisha kila mwaka kwa kuvuta moshi na chembe chembe zinazotokana na mkaa na kuni.

Alisema kupika kwa kutumia gesi ya Oryx huzuia ukataji miti, kwa hiyo husaidia kulinda mazingira, huku akieleza pia kutumia gesi ya Oryx huzuia wanawake kutumia muda mwingi kutafuta kuni na mkaa msituni.

Alisema: "Kupika kwa kutumia gesi ya Oryx ni kupika kwa haraka na kwa ufanisi zaidi; kwa hiyo, wanawake wataanda chakula kwa wakati na wanaume hawatalalamika juu ya kuchelewa kwa chakula kinachosababisha mizogo".

## HABARI KITAIFA

# Waandishi wa habari wakumbushwa kuzingatia amani kuelekea uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, amesema wakati nchi ikielekea kwenye uchaguzi, waandishi wa habari wana wajibu wa kuhamasisha ushiriki wenye kuheshimu amani, uchaguzi huru na wa haki.

Alisema, waandishi wa habari wanategemewa kupitia kalamu zao kuelimisha jamii, kuhamasisha amani na kuhakikisha hawawi sehemu ya kuivuruga nchi.

"Ni muhimu mkaelimisha jamii juu ya mchakato wa uchaguzi, wapate uelewa wa utofauti ya uchaguzi na ilani za vyama, lakini pia watambue umuhimu wa kujitokeza kupiga kura na thamani ya kura zao katika kuleta mabadiliko," alisema Matinyi.

Alikuwa akifungua mkutano wa Wanawake katika Vyombo vya Habari waliopita kwenye programu maaluma ya mafunzo ya uongozi (Women in News), uliofanyika jijini Dar es Salaam.



Alilitaka kundi hilo kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea katika chaguzi hizo zijazo kuanzia ndani ya vyama vyao vya siasa, uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Pia, kuhakikisha waandishi wa habari wanatumia kalamu zao vizuri kuibua changamoto zinazosababisha wanawake wengi wasijitokeze kugombea nafasi katika chaguzi mbalimbali.

"Kwa hakika, nchi yetu inahitaji wanawake katika nafasi za uongozi na mpaka sasa utendaji wa wanawake hao waliopo katika nafasi kubwa za uongozi hususani katika nchi yetu, unadhihirisha ubora wao, wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na Spika wa Bunge la Jamhuri, Dk.Tulia Ackson, ambaye kwa sasa anaongoza taasisi ya mabunge yote duniani," alisema Matinyi.

"Mtakumbuka kwamba katika falsafa ya Rais Samia ya R nne, ambazo ni Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahimilivu), Reforms (mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga upya). Kwa hiyo ni matarajio yangu kwamba wanawake mtatoa mchango mkubwa katika falsafa hizi."

Alisema idadi ya wanawake kwenye nafasi za kisiasa hususani ngazi ya wenyeviti wa vijiji, mtaa, wajumbe bado ni ndogo tofauti na ilivyo kwa wanaume.

"Hivyo, waandishi wa habari mna wajibu wa kuhamasisha ushiriki mkubwa na wenye kuheshimu amani, uchaguzi huru na wa haki, mtambue kuwa taifa linawategemea katika jambo hili. Tanzania inabeba ajenda ya kumuinua mwanamke katika ngazi mbalimbali na ndio maana Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kurejeshwa kwa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema Matinyi.

"Ninaamini kama Tanzania tumefanikiwa kuwa na kiongozi imara, shupavu na mchapakazi Rais Samia, basi vyombo vya habari vinapaswa kuiga mfano huu kwa kuwapa nafasi wanawake wenye uwezo kuongoza ili kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii."

Alisema kwa kuzingatia taaluma, ni vema kuhakikisha habari inayoandaliwa iwe imeshirikisha jinsia zote kuzungumzia yanayohusu mtazamo wa jamii nzima ili kuondoa utengano, ili kuijengea uwezo jamii yote kushiriki kwenye ujenzi wa taifa.

"Tumeshuhudia wanawake waliopewa nafasi kuongoza vyombo vya habari wamefanya vizuri sana. Mfano mzuri ni Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Radio One, Joyce Mhavile, huyu amefanya kazi kubwa na nzuri na kama sikosei ni zaidi ya miaka 20. Kwa hiyo tuwape nafasi," alisema Matinyi.

Aliipongeza WAN-IFRA kupitia programu yake ya 'Women in News' ambayo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuwapa maarifa waandishi wa habari wanawake na kutanua wigo wake kwa kutoa mafunzo kwa vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa usawa wa kijinsia.

Naibu Mkurugenzi na Mkurugenzi wa Afrika-WAN-IFRA/Women in News, Jane Godia, alisema upo umuhimu kwa vyombo vya habari kuwa na sera za jinsia na kuhakikisha wanawake wenye uwezo wanaaminiwa kuongoza vyombo vya habari.

Jane alisema uwapo wa sera hiyo, pia utatoa nafasi au fursa ya watu kutoa maoni yenye kuleta mabadiliko chanya ndani ya vyombo hivyo vya habari pamoja na kuleta ustawi na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu kwa makundi yote.


## TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha ( Uoneshaji ) ya Mwaka 2014

MWANGA HAKIKA BANK

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2024

| | Robo Mwaka wa sasa Mar-24 TZS '000 | Robo Mwaka Ulipitia Dec-23 TZS '000 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 3,183,050 | 3,768,172 |
| 2 Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,236,437 | 9,499,595 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za Serikali | 19,097,563 | 14,482,537 |
| 4 Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 48,574,135 | 35,090,700 |
| 5 Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 500,000 | 500,000 |
| 11 Mikopo Halisi iliyopo | 139,781,916 | 131,438,264 |
| 12 Mali Nyingine | 7,481,899 | 8,708,772 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 5,042,173 | 4,545,116 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **232,897,173** | **208,033,156** |
| **B. DHIMA** | | |
| 16 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 23,754,960 | 22,799,605 |
| 17 Amana za Wateja | 163,174,380 | 142,194,319 |
| 18 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 19 Amana Maalumu | - | - |
| 20 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 21 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 22 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 17,253 | 529,262 |
| 23 Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 24 Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi Mapato yalioingia ya kipindi | - | - |
| 25 Kijacho na Tozo Nyingine | 2,386,671 | 1,905,589 |
| 26 Dhima Nyingine | 2,881,148 | 4,370,215 |
| 27 Madeni | 7,068,593 | 7,132,688 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **199,283,005** | **178,931,678** |
| **30 MALI/{DHIMA} HALISI** | **33,614,168** | **29,101,478** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 18,315,792 | 17,011,676 |
| 32 Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 Mapato yaliyobakizwa | 12,089,802 | 5,587,954 |
| 34 Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 3,208,574 | 6,501,848 |
| 35 Akaunti zingine za Mtaji | - | - |
| 36 Stahiki ya wenye Hisa chache | - | - |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **33,614,168** | **29,101,478** |
| 38 Dhima zisizo dhahiri | 211,273,407 | 220,789,926 |
| 39 Mikopo chechefu | 2,324,338 | 2,322,957 |
| 40 Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,572,998 | 1,572,998 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| i Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 14% | 14% |
| ii ~~Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mik~~opo Ghafi | 1.6% | 1.7% |
| iii Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76% | 81% |
| iv Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60% | 63% |
| v Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89% | 80% |
| vi Ongezeko la Amana | 13% | 78% |
| vii Ongezeko la Mali | 12% | 79% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

**Zimesainiwa na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Jagjit Singh** | **Mkurugenzi Mtendaji** | **27/04/2024** |
| **Chomete Abdallah** | **Mkuu wa Idara ya Fedha** | **27/04/2024** |
| **Elifuraha Charles** | **Mkuu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani** | **27/04/2024** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Kuthibitishwa na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Eng. Ridhuan Mringo** | **Mwenyekiti wa Bodi** | **27/04/2024** |
| **CPA(T)Zukra Ally** | **Mjumbe wa Bodi** | **27/04/2024** |







### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2024

| | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-24 TZS '000 | Robo Mwaka Linganishi 31-Mar-23 TZS'000 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-24 TZS '000 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mar-23 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,343,633 | 4,299,523 | 7,343,633 | 4,299,523 |
| **2 Gharama za Riba** | **3,231,786** | **1,604,480** | **3,231,786** | **1,604,480** |
| 3 Mapato Halisi (1 kutoa 2) | 4,111,847 | 2,695,043 | 4,111,847 | 2,695,043 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| **5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo** | **-** | **(231,133)** | **-** | **(231,133)** |
| **6 Mapato yasiyo ya Riba:** | **1,985,302** | **1,672,388** | **1,985,302** | **1,672,388** |
| 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (19,363) | 215,572 | (19,363) | 215,572 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,675,047 | 1,400,120 | 1,675,047 | 1,400,120 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 329,618 | 56,697 | 329,618 | 56,697 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **2,378,575** | **2,391,202** | **2,378,575** | **2,391,202** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,103,776 | 947,887 | 1,103,776 | 947,887 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 20,879 | - | 20,879 | - |
| 7.3 Gharama nyingine | 1,253,920 | 1,443,315 | 1,253,920 | 1,443,315 |
| **8 Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,718,574** | **1,745,097** | **3,718,574** | **1,745,097** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (510,000) | (470,700) | (510,000) | (470,700) |
| **10 Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **4,228,574** | **2,215,797** | **4,228,574** | **2,215,797** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **4,228,574** | **2,215,797** | **4,228,574** | **2,215,797** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 124 | 113 | 124 | 113 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 938 | 372 | 938 | 372 |
| 15 Idadi ya Matawi | 7 | 7 | 7 | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | 1% | 1% | 1% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 10% | 5% | 10% | 5% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 25% | 40% | 25% | 40% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 7% | 6% | 7% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2023

| | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-24 TZS '000 | Robo Mwaka Ulipitia 31-Dec-23 TZS '000 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-24 TZS '000 | Limbikizo la Mwaka uliopita 31-Mar-23 TZS '000 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3,718,574 | 10,034,989 | 3,718,574 | 1,274,397 |
| **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | - | (8,268) | - | - |
| - Uchakavu wa Mali za Kudumu | (119,237) | 479,771 | (119,237) | 173,280 |
| - Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | (760,139) | 867,512 | (760,139) | 155,179 |
| - Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | - | - | - | - |
| - Hasara inayotarajiwa kutokana na IFRS 9 | - | - | - | (231,133) |
| - Marekebisho ya Mwanzo wa Mwaka | - | - | - | - |
| | **2,839,198** | **11,374,004** | **2,839,198** | **1,371,724** |
| - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | (3,407,391) | (4,369,695) | (3,407,391) | - |
| - Badiliko Halisi katika Mikopo | (8,343,652) | 11,374,004 | (8,343,652) | (12,583,741) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,226,873 | (4,369,695) | 1,226,873 | 508,794 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 21,935,416 | (50,751,929) | 21,935,416 | 22,556,058 |
| - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | (13,483,435) | (10,897,603) | (13,483,435) | 1,000,000 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,519,994) | 62,127,846 | (1,519,994) | 1,825,461 |
| | **(3,592,183)** | **3,112,928** | **(3,592,183)** | **13,306,572** |
| - Kodi Iliyolipwa | 510,000 | 2,143,884 | 510,000 | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(242,985)** | **16,630,816** | **(242,985)** | **14,678,295** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (497,057) | (2,426,148) | (497,057) | (2,249,159) |
| Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 9,086 | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Zisizoshikika | - | (73,847) | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughuliwa na Mawakala | (5,115,026) | (500,000) | (5,115,026) | (245,817) |
| Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughuliwa na Mawakala | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa** | **(5,612,083)** | **(2,990,909)** | **(5,612,083)** | **(2,494,976)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | (341,863) | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | 3,000,000 | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 1,304,116 | - | 1,304,116 | 4 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (64,095) | (366,400) | (64,095) | (163,932) |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha | **1,240,021** | **2,291,737** | **1,240,021** | **(163,928)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | (4,615,047) | 23,063,304 | (4,615,047) | 12,019,391 |
| Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 40,310,622 | 17,247,318 | 40,310,622 | 17,247,317 |
| **Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **35,695,575** | **40,310,622** | **35,695,575** | **29,266,708** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2024

| Robo Mwaka ulioishia 31.03.2024 | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Ziada ya Kisheria | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo 01.01.2024** | **17,011,676** | - | **12,089,802** | - | - | - | **29,101,478** |
| (Hasara) / Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,208,574 | - | - | - | 3,208,574 |
| Marekebisho madogo ya mwaka uliopita | - | - | - | - | - | - | - |
| Marekebisho madogo mwaka huu | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida itokanayo kwa kuungana kwa benki | - | - | - | - | - | - | - |
| Malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa Hisa | 1,304,116 | - | - | - | - | - | 1,304,116 |
| Kiwango cha Hisa zilizotolewa ndani ya mwaka | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho robo mwaka 31.12.2023** | **18,315,792** | - | **15,298,376** | - | - | - | **33,614,168** |
| **Robo mwaka iliyopita 31.12.2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo 01.10.2023** | **17,111,834** | - | **5,587,954** | - | - | - | **22,699,788** |
| (Hasara) / Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,501,848 | - | - | - | 6,501,848 |
| Marekebisho madogo ya mwaka uliopita | - | - | - | - | - | - | - |
| Marekebisho madogo mwaka huu | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida itokanayo kwa kuungana kwa benki | - | - | - | - | - | - | - |
| Malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kiwango cha Hisa zilizotolewa ndani ya mwaka | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.12.2023** | **17,111,834** | - | **12,089,802** | - | - | - | **29,201,636** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF kuficha jina usajili tata Yanga kunazua maswali

**SHIRIKISHO** la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Aprili 12, mwaka huu, lilitoa taarifa kwa umma kupitia mtandao wake wa kijamii, likieleza kupokea taarifa kutoka Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), juu ya kufungiwa kwa Klabu ya Yanga kufanya usajili kutokana na kukiuka Kanuni ya Uhamisho.

TFF, ilisema uamuzi huo ulifanywa na FIFA baada ya Klabu ya Yanga kukiuka kile kilichoitwa Annexe 3 ya Kanuni ya Uhamisho (RSTP) ya shirikisho hilo. Ikasema Yanga haikuingiza uthibitisho wa malipo wa uhamishowa mchezaji husika katika usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.

Ikaelezwa kuwa klabu hiyo ilitakiwa kutekeleza matakwa ya kikanuni na kuwasilisha taarifa kwa Sekretarieti ya Nidhani ya FIFA ambapo suala hilo limefikishwa kwa ajili ya hatua zaidi.

Kwa ujumla ukisoma kwa umakini taarifa hiyo ya TFF, ina mapungufu kwani haikuandika jina la mchezaji ambaye amesababisha klabu hiyo kufungiwa kusajili kitu ambacho si cha kawaida kwa shirikisho hilo kila linapotoa taarifa hizo za Fifa.

Hatudhani hata kidogo kama FIFA haikuwaambia TFF ni mchezaji gani, hivyo ni wazi yenyewe ndiyo imeamua kuficha jina hilo na hapo ndipo wadau wa soka wanakuwa na maswali mengi ya kujiuliza ni kwa sababu gani.

Hofu hiyo inakuja kutokana na utaratibu wa TFF kuwa wa wazi kila inapotokea klabu za soka nchini kuadhibiwa FIFA.

Ni wiki iliyopita tu TFF hiyo hiyo imetoa taarifa kutoka FIFA juu ya kufungiwa kwa Klabu ya Tabora United kutokana na kumtumia mchezaji Jean Didie Touya. mbona haijaficha jina?

Huko nyuma Yanga ilikuwa na mgogoro wa wachezaji mbalimbali kama Bernard Morrison, Gael Bigirimana na aliyekuwa kocha wake, Luc Eymael, lakini haikufichwa, kila mmoja alilijua Yanga imeshtakiwa na kocha au mchezaji gani.

Hata klabu ya Simba ilikumbana na adhabu kama hiyo, ambapo TFF ilitoa taarifa yake Novemba 23, mwaka jana, juu ya klabu hiyo kufungiwa mpaka itakapotekeleza madai ya Klabu ya Teungueth ya Senegal kuhusu mchezaji Pape Sakho.

Klabu hiyo ilifungua madai dhidi ya Simba ikidai malipo ya mauzo ya mchezaji, kama walivyokubaliana kwenye mkataba wa mauziano ya Sakho, ambapo klabu hiyo ilitakiwa kuilipa timu hiyo baada ya kumpiga bei klabu ya Quevilly Rouen Metropole ya Ufaransa.

Wadau na mashabiki wa soka wanaiona TFF kama kuna kitu ambacho inakificha kwa maslahi ya Yanga, jambo ambalo tunaona ipo haja ya shirikisho hilo kuweka kila kitu hadharani ili kutoonekana linaegemea upande fulani katika maamuzi yake.


Hoja kuntu, inakuja kwa kile walichohoji kwa nini mchezaji huyo aliyesababisha Yanga kufungiwa asitajwe, badala yake kumficha? Hii inatia mashaka kwa viongozi wa TFF ambao wamejipambanua kuendesha soka bila upendeleo na ubaguzi. Nini kinalindwa hapo?

Sisi tunaamini katika uwazi, na katika hilo, TFF walipaswa wataje jina la mchezaji ili kila mdau wa soka ajue baada ya hiki nini kinaendelea na kama ni miongoni mwa wachezaji waliocheza mechi za Ligi Kuu wakiwa hawajakamilisha kanuni hiyo, nini mustakabali wake?

Nipashe tunashangaa kuona hata wale wanajipambanua kama wachambuzi wa soka wakipiga kelele katika kila kinachotokea kwenye mpira wa miguu nchini, katika hili wamekuwa kimya kama wamemwagiwa maji ya baridi.

Wachambuzi ambao wamekuwa wakijadili hata tetesi za usajili, au chapisho tu la mtu binafsi, kufanya vibaya kwa baadhi ya klabu, ubora na udhaifu wa makocha mpaka uwekezaji wa klabu nchini, lakini masuala nyeti kama haya wamekuwa kimya.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk.Doto Biteko alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki bungeni alipokuwa akihitimisha hoja ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25.

"Niwaombe Watanzania tuache kuwa madalali wa kujinyima faida kama nchini, hapa kwenye EACOP kanuni yetu ipo wazi kwamba kazi anazoweza kufanya mtanzania afanye na siyo mgeni, vinatokea vikampuni vya kigeni vinamtafuta mtanzania mmoja anatoa NIDA na nyaraka zake inasajiliwa kampuni ni share company, mtanzania anapewa hela kidogo." alisema

Alipongeza EWURA kwa usimamizi mzuri wa ushiriki wa kampuni za ndani kwenye mradi huo na kuwaondoa wote waliofanya udalali.

Dk. Biteko alisema: "Tutaendelea na kazi ya kuwachambua, haiwezekani eti kujenga barabara ya vumbi inayohitaji mitambo ambayo Watanzania wanayo, haitawezekana chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwasababu tunataka Watanzania wanufaike na miradi hii".



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk Khamis Mkanachi (watatu kulia) akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk Ally Laay (wanne kushoto) wakifungua kitambaa ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa madarasa mawili ya Shule ya Msingi Isabe, iliyopo katika kijiji cha Bukulu, Wilayani Kondoa, yaliyojengwa kwa ufadhili wa Benki ya CRDB na yenye thamani ya shilingi Milioni 40. Hafla hiyo imefanyika Aprili 25, 2024 na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, Benki ya CRDB pamoja na Wananchi wa eneo hilo na maeneo ya jirani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanachama TAPEI kuwezeshwa kuboresha elimu shule binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono juhudi za kuboresha elimu nchini, Benki ya CRDB imetia saini mkataba wa ushirikiano na Chama cha Wawekezaji katika Elimu Tanzania (TAPIE), utakaowezesha wanachama wake kupata mikopo nafuu ya kuboresha miundombinu na kuwezesha uendeshaji wakati wote.

Mkataba huo uliotiwa saini mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa tano wa mwaka wa TAPEI uliofunguliwa na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko.

Akizungumza na wajumbe waliohudhuria mkutano mkuu huo, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa alisema benki inatambua changamoto wanazokutana nazo wamiliki binafsi wa shule, hivyo imechukua hatua za kusaidia kuzitatua ili kuwa na mazingira rafiki kwa wanafunzi kusoma na kujifunza.

Raballa alisema shule nyingi zipo kwenye maeneo ambayo hayajarasimishwa, jambo linalonyima wamiliki uwezo wa kukopa kutokana na kutokidhi vigezo vya dhamana.

Hivyo alisema Benki ya CRDB imewaletea suluhisho kwa kuruhusu kukopa fedha zitakazowezesha urasmishaji maeneo yao ili kupata hati ya wizara itakayowaruhusu kukopa ili kuimarisha biashara zao.

Wakati wamiliki wakipewa mkopo wa uwekezaji wanaoweza kuurejesha mpaka kwa miaka saba, Raballa alisema walimu na wafanyakazi wa shule binafsi nao wanaweza kupata mkopo kwa ajili ya kufanikisha mambo yao binafsi.

Alisema mikopo ya wafanyakazi inajumuisha 'salary advance' ambao ni mahsusi kwa wale ambao mishahara yao inapitia Benki ya CRDB ambao wanaweza kupata mpaka asilimia 50 ya mshahara wao na wakalipa ndani ya siku 30 pamoja na mkopo wa binafsi unaofika mpaka Sh. milioni 100 zinazoweza kurejeshwa kwa mpaka miaka minane.

Rais wa TAPIE, Mahmoud Mringo alisema hadi sasa kuna zaidi ya shule 6,362 zinazojumisha za awali 2,364, za msingi 2,270 na sekondari 1,728 zinazomilikiwa na watu binafsi, mashirika ya dini na yasiyo ya dini, majeshi na jumuiya za wazazi.

Alisema shule hizo zimedahili wanafunzi 1,020,772 kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita na zimeajiri walimu 59,445 na wataalamu wengine zaidi ya 100,000 wenye taaluma na ujuzi mbalimbali kama wahasibu, madereva, wasimamizi na walezi wa wanafunzi, walinzi na wapishi.

Akifungua mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alipongeza juhudi za sekta binafsi kuchangia kuboresha elimu nchini kwamba zinaifanya jamii iwe na mchango zaidi katika kukuza uchumi.

## Wakulima alizeti wapigwa msasa kanuni bora za uzalishaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Ilonga kilichopo Kilosa mkoani Morogoro kimeendelea kutoa elimu kwa wakulima nchini kuhusu kanuni bora za uzalishaji wa alizeti.

Mtafiti na Mhaulishaji wa Teknolojia za Kilimo kutoka TARI ILONGA, Baraka Daniel, akizungumza na wakulima na viongozi wa Kijiji cha Mdilu, Kata ya Mwasauya Halmashauri ya Singida katika Siku ya Mkulima wa Alizeti, alisema mbali na mbegu ya record mbegu nyingine mpya zilizofanyiwa utafiti ambazo zimetambulishwa kwa wakulima waanze kuzitumia ni TARI ILO-19 na TARI NAL-19.

Alisema wanahamasisha matumizi ya mbegu hizo kwa sababu zinastahimili mabadiliko ya tabianchi, bei ya wastani ambayo wakulima wengi wanamudu kununua pia zina tija katika uzalishaji.

Alisema Mkoa wa Singida ni kati ya mikoa nchini inayolima alizeti lakini tija ni ndogo kutokana na wakulima wengi kutumia mbegu za kienyeji ambazo hazijafanyiwa utafiti.

Mratibu wa Upimaji wa Afya ya Udongo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Benny Joel, alisema katika kuadhimisha siku hiyo wanatoa elimu kwa wakulima ili kutambua umuhimu wa upimaji afya ya udongo kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Alisema awali wakulima walikuwa wanapata kati ya gunia tano hadi saba kwa ekari moja kwasababu upimaji wa udongo ulikuwa haufanyiki na pia mbegu walizokuwa wanatumia wakulima ni za kienyeji na pia matumizi ya mbolea hayakuwepo.

Kwa upande wao wakulima wa alizeti Maria Mandi na Rashid Idd kutoka Kijiji cha Mdilu walisema tangu waanze kutumia mbegu ya alizeti aina ya record hivi sasa wanapata gunia 12 hadi 14 kwa ekari moja wakati awali walipokuwa wanatumia mbegu za kienyeji walikuwa wanapata gunia nne hadi tano.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mdilu, Samson Samweli, alisema mbegu ya record imekuwa mkombozi kwa wakulima wa kijiji chake kutokana na kuongeza uzalishaji ambao kupitia zao hilo wameinua hali zao za maisha.

TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
TACOBA
"Our Bank for Our Development"

# BENKI YA WANANCHI TANDAHIMBA

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha '(Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE - 31 MACHI, 2024

(Kiasi kwa Shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/03/2024 | Robo mwaka iliyopita 31/12/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 124,217 | 263,191 |
| 2. | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 187,101 | 1,566,968 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 3,289,228 | 2,854,476 |
| 12 | Mali Nyingine | 170,567 | 352,194 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 141,269 | 155,440 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **3,912,382** | **5,192,269** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,257,569 | 1,711,275 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo /Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 13,906 | 131,665 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 53,722 | 91,143 |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,464 | 50,542 |
| 28 | Madeni | 200,000 | 871,147 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **1,555,661** | **2,855,772** |
| 30 | **MALI/ DHIMA HALISI (16 kutoa 29)** | **2,356,721** | **2,336,497** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 4,483,228 | 4,483,228 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yalibakizwa | (2,250,761) | (2,327,779) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 12,400 | 65,901 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 111,854 | 115,147 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,356,721** | **2,336,497** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 67,779 | 80,748 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 46,352 | 51,555 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 60.2% | 45.0% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.0% | 2.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi Halisi na Jumla ya Amana | 265.2% | 169.8% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 84.1% | 55.0% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.9% | 85.2% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -26.5% | 96.3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -24.6% | 25.8% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 31 MACHI,2024

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/03/2024 | Robo mwaka Iliyopita 31/03/2023 | Mwaka wa Sasa 31/03/2024 | Mwaka Uliopita 31/03/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Riba | 137,291 | 102,669 | 137,291 | 102,669 |
| 2. | Gharama za Riba | (24,257) | (1,007) | (24,257) | (1,007) |
| 3. | **Mapato Halisi ya Riba ( 1 kutoa 2)** | **113,034** | **101,662** | **113,034** | **101,662** |
| 4. | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 6,734 | 7,657 | 6,734 | 7,657 |
| 6. | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **44,701** | **31,031** | **44,701** | **31,031** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 44,701 | 31,031 | 44,701 | 31,031 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7. | **Gharama Zisizo za Riba** | **(146,755)** | **(173,573)** | **(146,755)** | **(173,573)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (45,258) | (64,057) | (45,258) | (64,057) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (101,497) | (109,516) | (101,497) | (109,516) |
| 8. | **Faida / (Hasara) Halisi ya Uendeshaji** | **17,714** | **(33,223)** | **17,714** | **(33,223)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (5,314) | 9,967 | (5,314) | 9,967 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **12,400** | **(23,256)** | **12,400** | **- 23,256** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 12,400 | (23,256) | 12,400 | **(23,256)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 16 | 15 | 16 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 3 | (5) | 3 | -5 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i)Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.8% | -3.8% | 0.5% | -3.8% |
| | (ii)Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.1% | -4.1% | 0.5% | -4.1% |
| | (iii)Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 93.0% | 130.8% | 93.0% | 130.8% |
| | (iv)Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.3% | 13.0% | 12.3% | 13.0% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA - 31 MACHI, 2024

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya | Mapato yaliyobakiz | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa-31/03/2024** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 4,483,228 | - | (2,261,877) | 812 | - | 114,335 | **2,336,497** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,200 | - | - | - | **6,200** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | **0** | **(0)** | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | **(3,293)** | **(3,293)** |
| Mengineyo | - | - | **17,317** | - | - | - | **17,317** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **4,483,228** | **-** | **(2,238,360)** | **812** | **-** | **111,042** | **2,356,721** |
| **Mwaka uliopita-31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **4,483,228** | - | **(2,339,556)** | **173** | - | **153,306** | **2,297,150** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 65,901 | - | - | - | **65,901** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | **(639)** | **639** | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | **12,417** | - | - | **(38,972)** | **(26,555)** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **4,483,228** | **-** | **(2,261,877)** | **812** | **-** | **114,335** | **2,336,497** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 31 MACHI, 2024

(Kiasi kwa Shilingi Maelfu)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 31/03/2024 | Robo Mwaka Iliyopita 31/12/2023 | Mwaka wa Sasa 31/03/2024 | Mwaka Uliopita 31/03/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 17,714 | 105,317 | 17,714 | (33,223) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara katika Mali | 4,790 | 24,136 | 4,790 | 12,610 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (397,563) | 222,842 | (397,563) | (266,422) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi katika Amana | (453,706) | 835,811 | (453,706) | (443,155) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | - | - | - |
| | za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (175,258) | 79,629 | (175,258) | 31,614 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 181,627 | (173,482) | 181,627 | (14,212) |
| | - Kodi iliyolipwa | (3,000) | (31,750) | (3,000) | 3,000 |
| | - Mengineyo (bainisha) | (22,297) | 8,505 | (22,297) | (98,868) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(847,694)** | **1,071,008** | **(847,694)** | **(808,655)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | Gawio Lilopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (3,821) | - | 62,298 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji** | **-** | **(3,821)** | **-** | **62,298** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lilolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (671,147) | 2,188 | (671,147) | 500,000 |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **(671,147)** | **2,188** | **(671,147)** | **500,000** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,518,841) | 1,069,375 | (1,518,841) | (246,358) |
| | Fedha Taslimu na Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,830,159 | 760,784 | 1,830,159 | 889,242 |
| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **311,318** | **1,830,159** | **311,318** | **642,884** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI,2024

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita**

| | Tarehe | Saini |
|---|---|---|
| Yahya J. Kiyabo<br>**Meneja Mkuu** | 25/04/2024 | |
| Julius J. Sawaya<br>**Mkuu wa Fedha** | 25/04/2024 | |
| Aloyce Leonard<br>**Mkaguzi wa Ndani** | 25/04/2024 | |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2016, na zinaonesha hali halisi.

| | Tarehe |
|---|---|
| Mohamed N. Mwinguku<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | 25/04/2024 |
| Mariam S. Mwanzalima<br>**Mjumbe wa Bodi** | 25/04/2024 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

| Sn | BANK CHARGES 2023 Transactions | Description | New Rates 2024 VAT Exclusive | VAT Inclusive |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Account Maintenance Fee** | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 2,500 | 2,950 |
| | Company Savings | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | **Group saving** | | - | - |
| | Amcos Collection | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | Amcos Business | Per Month | Free | Free |
| | Local council | Per Month | 13,000 | 15,340 |
| | Group saving | Per Month | 3,500 | 4,130 |
| 2 | **Min account Opening** | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a |
| 3 | **Min operating Balance** | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a |
| 4 | **Cash withdral Over the counter** | | | |
| | From TZS 1,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-9,999 | Per transaction | 750 | 885 |
| | From TZS 10,000-19,999 | Per transaction | 1,200 | 1,416 |
| | From TZS 20,000-39,999 | Per transaction | 1,650 | 1,947 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,500 | 4,130 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 4,500 | 5,310 |
| | From TZS 200,000-299,999 | Per transaction | 5,500 | 6,490 |
| | From TZS 300,000-599,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 600,000-799,999 | Per transaction | 7,000 | 8,260 |
| | From TZS 800,000-999,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 1,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 3,000,000-4,999,999 | | 9,500 | 11,210 |
| | 5,000,000 - Above | | 9,500+0.12 % of excess max 170,000 | 9,500+0.12 % of excess max 170,000 |
| | Mwana A/C cash withdrawal exceeding 3rd transaction per annum | Per transaction | 3,000 | 3,540 |
| 5 | **Cash withdral - TACOBA Agency Banking** | | | |
| | From TZS 0-499 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 500-999 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 1,000-1,999 | Per transaction | 250 | 295 |
| | From TZS 2,000-2,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 3,000-3,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 4,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-6,999 | Per transaction | 700 | 826 |
| | From TZS 7,000-9,999 | Per transaction | 700 | 826 |
| | From TZS 10,000-14,999 | Per transaction | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 15,000-19,999 | Per transaction | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 20,000-29,999 | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 30,000-39,999 | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,200 | 3,776 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 3,950 | 4,661 |
| | From TZS 200,000-239,999 | Per transaction | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 240,000-299,999 | Per transaction | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 300,000-399,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 400,000-499,999 | Per transaction | 6,800 | 8,024 |
| | From TZS 500,000-599,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 600,000-699,999 | Per transaction | 7,700 | 9,086 |
| | From TZS 700,000-799,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 800,000-899,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 900,000-999,999 | Per transaction | 8,500 | 10,030 |
| | From TZS 1,000,000-1,999,999 | Per transaction | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 2,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 3,000,000-3,999,999 | Per transaction | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 4,000,000-4,999,999 | Per transaction | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 5,000,000-5,999,999 | Per transaction | 10,000 | 11,800 |
| | From TZS 6,000,000-6,999,999 | Per transaction | 11,000 | 12,980 |
| | From TZS 7,000,000-7,999,999 | Per transaction | 12,500 | 14,750 |
| | From TZS 8,000,000-8,999,999 | Per transaction | 14,000 | 16,520 |
| | From TZS 9,000,000-9,999,999 | Per transaction | 15,000 | 17,700 |
| | From TZS 10,000,000 & Above | Per transaction | 15,000 | 17,700 |
| 6 | **Activation of Dormant Accounts** | | | |
| | All other accounts | Free | Free | Free |
| | Saving account of personal loan customers | Per account | Free | Free |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | **Closing of Account** | | | |
| | Saving account | Per account | 5000 | 5900 |
| | All other accounts | Per account | 10000 | 11800 |
| 8 | **Inter-Bank (Outward Funds Transfer)** | | | |
| | TISS | Per transaction | 10000 | 11800 |
| | **Inter-Bank (Inward Funds Transfer)** | | | |
| | Internal Transfer | Per transaction | 1000 | 1180 |
| 9 | **Cards** | | | |
| | **New Cards** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 |
| | **New Cards due to expired** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 |
| | **Peplacement due to lost/spoiled** | | | |
| | Tacoba card | Per card | 10,000 | 11,800 |
| | Korosho card | Per card | 22,000 | 25,960 |
| | Annual card fee All Cards | per card | 10,000 | 11,800 |
| 10 | **Account statements** | | | |
| | Interim statement per month | per transaction | Free | Free |
| | Quartely statement | per transaction | 3,000 | 3,540.00 |
| | Adhoc from 4 up to 12 month | per transaction | 15,000 | 17,700.00 |
| | Adhoc above 12 month | per transaction | 20,000 | 23,600 |
| 11 | **Salary and Bulk payment** | | | |
| | Salary and Bulk payment fee | per transaction | 3,000 | 540 |
| | Transfer to other Banks | per transaction | 5,000 | 900 |
| | Balance enquiry | per request | Free | Free |
| 12 | **Information search** | | | |
| | For information up to 12 past months | per document | 50,000 | 59,000 |
| | For information of 1 to 5 past years | per document | 80,000 | 94,400 |
| | For information above 5 years | per document | 100,000 | 118,000 |
| | CCTV Image retrieve | Per request | 100,000 | 118,000 |
| 13 | **Introduction Letter and certificate of Balance** | | | |
| | Cerfificate of balance | per item | 50,000 | 59,000 |
| | status report | per report | 50,000 | 59,000 |
| | Visa recommendation | per item | 50,000 | 59,000 |
| | Any other introduction | per item | 50,000 | 59,000 |
| | Bank statement requested by other banks | per item | 50,000 | 59,000 |
| 14 | **Loan Fees** | | | |
| 1 | **MSE** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% | |
| | Facility Fee | | 1% | |
| | Legal documentation fee | | 1% | |
| 2 | **AGRICULTURE LOANS** | | | |
| | Loan fee | 0-999,999 | 100,000 | 118,000 |
| | Loan fee | 1mn - 1,999,999 | 200,000 | 236,000 |
| | Loan Application fee | 2mn and above | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | |
| 3 | **PERSONAL LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 0.55% MIN 55,000 | |
| | Facility Fee | | 1% MIN 90,000 | |
| | Legal documentation fee | | Free | |
| 4 | **GROUP LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | |
| 5 | **ASSET FINANCING LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 1% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% on Loan amount | |
| 6 | **CHAPCHAP LOAN** | | | |
| | Loan Application fee | | Free | |
| | Facility Fee | | 0% | |
| | Legal documentation fee | | Free | |
| 15 | **charges on early loan payment** | | | |
| | Salary loan | | 5.9% min 500,000 | |
| | MSE business loan | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | |
| | Agriculture loan | | Free | |
| | Other segment | | 3% on the unpaid amount | |
| | Restructuring Fee | | 2% min 150,000 | 177,000 |
| 16 | **Cheque Book order** | | | |
| | Per leaf - 100 | | 1,000 | 1,180 |





## Waziri ataja dawa kupunguza vifo mama, mtoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui amewataka wajawazito kuhudhuria kliniki mapema ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza katika kikao kazi cha kujadili, kuendeleza mpango wa kumlinda mama na mtoto (M-MAMA Zanzibar) visiwani Zanzibar.

Alisema kuwa vifo vingi vya mama na mtoto vinatokana na baadhi ya kinamama kutohudhuria kliniki mapema wakati wa ujauzito na kujifungua nyumbani, jambo ambalo linasababisha madhara mbalimbali ikiwemo kifo.

Aidha aliwataka wanaume kuongozana pamoja na weza wao kuhudhuria kliniki kipindi cha ujauzito ili kujua maendeleo ya mama na mtoto.

"Tusione aibu wanaume wenzangu kuongozana na wake zetu kuhudhuria kliniki na tuwe mstari wa mbele katika kuwahimiza na kuwashajihisha kuhudhuria mapema tangu mimba inapotunga badala ya kusubiri muda wa kujifungua" alisema Mazrui.

Naye Mwenyekiti wa kikosi kazi cha mpango wa M-MAMA Zanzibar, Mohammed Habib, alisema lengo la mpango huo ni kuhakikisha vifo vya mama na mtoto vinapungua Zanzibar.

Msimamizi wa mpango wa M-MAMA kitaifa kutoka Vodafone, Rahma Bajuni, alisema ni wajibu wa kila mwanafamilia kuhakikisha anautumia mpango huo na kumuwahisha hospitali mama na mtoto ili kuokoa maisha yao.

Kikaokazi cha kujadili mpango wa M-MAMA kiliwashirikisha wataalamu na wadau mbalimbali wa mama na mtoto visiwani hapa.

# SMZ, Saudi Arabia kuendeleza ushirikiano katika miradi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amehakikishia Serikali ya Saudi Arabia ushirikiano mzuri na serikali yake, hasa kwenye miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Yahya Ahmad Okeish na ujumbe wake kwa lengo la kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya nchi mbili hizo.

Dk. Mwinyi alisema, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni mnufaika mkubwa wa mfuko wa Saudia na Quwait kwenye miradi yake ya maeneleo kupitia ushirikiano mzuri uliopo baina ya mataifa hayo.



Aidha, Dk. Mwinyi aliishukuru na kuipongeza Serikali ya Saudi Arabia kwa ushirikiano wake na Tanzania hususani kuipatia Zanzibar zawadi mbalimbali inazozituma kwa watu wa Zanzibar ikiwemo tende wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Katika salamu zake kwa Tanzania, Balozi Okeish alipongeza mafanikio makubwa yaliyofikiwa na taifa hioi kwa kutimiza miaka 60 ya muungano wake baina ya Tanganyika na Zanzibar sambamba na kuuombea mafanikio zaidi muungano huo.

Pia, Balozi Okeish alisifu ushirikiano wa diplomasia uliopo baina ya Saudi Arabia na Tanzania ikiwemo Zanzibar pamoja na kusifu tamaduni za pande mbili hizo.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi (kulia) akimkabidhi jiko la gas mmoja wa wafanyabiashara wanawake maarufu kama Mama Ntilie, Sauda Khamis wakati wa mafunzo ya uchumi shirikishi ya Mwanamke Shujaa yaliofanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki. Zaidi ya wanawake 1,400 kutoka Unguja na Pemba walifaidika na mafunzo hayo pamoja na vitendea kazi kama jiko pamoja na mtungi wa gesi, mafriji, viti na meza kutoka kampuni ya Coca-Cola Kwanza. Wengine ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii Zanzibar Riziki Pembe (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji Coca-Cola Kwanza Unguu Sulay (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yataja sababu kuendeleza kilimo cha mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema imeamua kuendeleza kilimo cha mwani ili kuwapa tija wakulima wa zao hilo.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mipango Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Mohammed Said Khamis, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji wa matumizi ya mwani visiwani hapa.

Alisema kwa kuthamini zao hilo serikali iko mbioni kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu kwa zao hilo ili kulipa thamani ambapo kiwanda hicho kipo eneo la Chamangwe Kisiwani Pemba.

Alisema uzinduzi wa programu ya uhamasishaji wa zao la mwani Zanzibar na Tanzania Bara ni muhimu katika kuimarisha sekta hiyo kwa maslahi ya Watanzania wote.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeona ipo haja ya kuhamasisha matumizi ya mwani ili kulipa thamani zao hilo.

Aidha, alisema kuwa utafiti mbalimbali zinaonesha kuwa mwani ni zao pekee lenye virutubisho vingi ukilinganisha na mazao mengi ya baharini, hivyo kuna kila sababu kwa wananchi kulithamini zao hilo.

"Matumizi ya mwani na bidhaa zake hujenga jamii yenye afya bora na kusababisha kuimarika kwa kinga ndani ya mwili na kuepuka kutumia dawa zisizo na lazima na kuipunguzia serikali gharama za kuagiza dawa,"alisema.

Alisema ili kuhakikisha wanakombolewa wakulima wa zao hilo na kuondokana na hali duni ya kiuchumi wizara imechukua juhudi mbalimbali ikiwemo kuwapatia dhana bora za kilimo ikiwemo boti, utowaji wa taaluma, teknolojia mpya ya ukulima wa zao hilo ili kuleta tija kwa walengwa.

Alisema serikali imeshajenga viwanda vya kusarifu mwani vitakavyosaidia katika kumkomboa mkulima wa mwani kwa kuongeza kipato.

Alisema kiwanda hicho kinauwezo wa kusarifu wastani wa tani 30,000 kwa mwaka, kinathamani ya shilingi bilioni 8.5.

Mraitibu wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (IFAD), Amina Ussi Khamis alisema uzinduzi huo utasaidia kuwainua wakulima wa mazao ya baharini kwa kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao yao na kuinua kipato chao.

Alisema licha ya kulimwa kwa zao hilo kwa kasi kubwa lakini bado kunahitajika jitihada zaidi ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyopo hivi sasa.

Naye Katibu wa Ushirika wa Kilimo Hai Zanzibar, Semeni Mohammed Salum, alisema mwani ni moja ya mazao ya kimkakati, hivyo serikali inaungana na wakulima wa zao hilo katika kuwapa elimu ili kuwainua kiuchumi.

Alisema katika kufikia malengo ya wakulima hao serikali imeandaa mpango wa kuwafundisha wakulima utumiaji wa mbegu bora za mwani ili kuendana na mabadiliko ya tabianchi.

# Tatizo mbolea kuwafikia wakulima kushughulikiwa

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

CHANGAMOTO ya mbolea ya kutowafikia kwa wakati wakulima mkoani Kigoma imeanza kushughulikiwa na mamlaka husika kwa kuongeza idadi ya mawakala wa vituo vya kutolea huduma kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024.

Mshauri wa kilimo mkoani hapa, James Peter amebainisha hayo katika mafunzo ya wakala wa mbolea kutoka mikoa ya Kigoma, Shinyanga, Singida na Tabora kuhusu rutuba ya udongo na matumizi bora ya mbolea yaliyoandaliwa na kampuni ya mbolea ya Minjingu yaliyofanyika wilayani Kasulu.

Alisema kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 mkoa mzima wa Kigoma ulikuwa na mawakala watano jambo lililokuwa changamoto kwa wakulima kupata mbolea ya ruzuku kwa wakati hali iliyofanya serikali ya mkoa huo kuongeza mawakala hadi kufikia 56 na vituo 64 kwa msimu wa mwaka 2023/2024 ili kupunguza changamoto hiyo na kuwezesha wakulima kupata mbolea ya ruzuku katika maeneo yao.

"Mfumo wa ruzuku ya mbolea ulianza kutekelezwa mwaka 2022/2023, na sasa tupo msimu wa pili, mara baada ya msimu wa ruzuku kuanza, mahitaji ya mbolea yalikuwa makubwa kwa wakulima, kwa mfano kwa msimu huo tulioanza nao tulikuwa na tani 31,555 za mbolea zilizotumiwa na wakulima na kuongezeka hadi kufikia tani 37,525, hii inaonesha namna gani wananchi walipokea mabadiliko kwaajili ya kilimo chenye tija," alisema Peter.

Aidha, alisema kutokana na ongezeko la mawakala na vituo vya kuuzia mbolea, uzalishaji umekua kutoka tani milioni 2.3 kwa msimu wa 2022/2023, na msimu huu wanatarajia kupata tani milioni 3.5 za uzalishaji wa mazao ya chakula na kuwa na uhakika katika usalama wa chakula hicho.

Peter alisema wanatarajia kuongeza mawakala wa mbolea kwa kuhusisha vikundi vya ushirika (AMCOS) ili wakulima waweze kupata huduma wakiwa katika maeneo yao ndani ya kijiji au kata ikiwa ndio lengo kuu la serikali.

Mshindo Msolla, Mkurugenzi wa masoko kutoka kampuni ya mbolea ya Minjingu, aliwataka mawakala wa mbolea kuwa waadilifu katika biashara yao ili kuleta tija inayohitajika katika kilimo.

"Naomba mawakala wachukulie biashara ya kuuza pembejeo kuwa ni ajira ya kudumu, wawe waaminifu katika kuwahudumia wakulima na wawaelimishe wakulima kupitia shamba darasa kwa kuwaelekeza kipimo sahihi cha matumizi ya mbolea," alisema Msolla.

Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea mkoani Kigoma (TFRA), Obadiah Oswad, aliwataka mawakala kuendelea kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na mamlaka hiyo katika utoaji wa huduma za mbolea kwa wakulima na kuwakumbusha wakulima kujiandikisha ili kupata namba ya utambulisho itakayowawezesha kupata mbolea ya ruzuku.

Alisema kwa mawakala watakaokwenda kinyume na taratibu watafungiwa leseni zao na kulipa faini mbalimbali kutokana na aina ya kosa walilolifanya kulingana na sheria.

Mawakala katika mafunzo hayo, Yahya Ramadan, Mwenyekiti wa AMCOS ya Mnang'ano kutoka Singida alisema ili wasiendelee kukosea maelekezo ya matumizi ya mbolea na majina yake yawekwe kwenye lugha nyepesi ili mkulima aelewe kwa urahisi.

# Morogoro kuhamasisha matumizi ya mbolea

**Na Renatha Msungu,** MOROGORO

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Mussa Ally Mussa, ameahidi mkoa wake kushiriki uhamasishaji matumizi ya mbolea na kusaidia kuondoa imani potofu kuwa udongo wanaoulima una rutuba ya kutosha na kusababisha matumizi hafifu ya mbolea.

Amesema wakulima wengi wanaamini udongo wao una rutuba kutokana na kupokea inayosafirishwa kutoka milimani wakati wa mvua kubwa.

Alisema hayo Aprili 22, mwaka huu alipokuwa akizungumza na Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), ilipofanya ziara ofisini kwake iliyolenga kuhamasisha ofisi za mkoa kushiriki uhamasishaji matumizi ya mbolea pamoja na kupima afya ya udongo kupitia vifaa vilivyogawiwa na Wizara kwa Maofisa Ugani wa kata zote nchini.

changamoto nyingine ni uelewa mdogo wa matumizi sahihi ya mbolea na jiografia ya mkoa ni suala jingine linalosababisha matumizi hayo kuwa hafifu.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya TFRA, Dk. Anthony Diallo, aliiomba Ofisi ya Mkoa kuhimiza maofisa ugani ndani ya mkoa huo kupima afya ya udongo na kuwasilisha taarifa za upimaji huo ili kuwasaidia wakulima kujua aina ya mbolea wanayopaswa kutumia kulingana na mahitaji ya udongo na hivyo kuongeza tija.

Pia, aliomba uongozi wa mkoa huo kuwashirikisha wafanyabiashara wa mbolea kwenye vikao vya pembejeo ili wapate maoni yao kabla ya kuwasilisha TFRA ili yazingatiwe wakati wa kupanga bei elekezi na hivyo zilingane na umbali wa maeneo wanakofikisha bidhaa hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, aliuomba uongozi wa mkoa kuhimiza wananchi wake kujisajili ili waweze kunufaika na ruzuku ya mbolea inayotolewa na serikali ili kuwapa ahueni ya gharama za uzalishaji wakulima.

Alisema mpaka Aprili 14, mwaka huu jumla ya wakulima 138,538 wamesajiliwa kwenye mfumo wa mbolea za ruzuku na wanufaika wa mpango huo ni 13,653 walionunua tani 10,808.15.

Akiwasilisha ombi la wafanyabiashara wa mbolea katika kikao baina yao na TFRA, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Mbolea, Gerold Mlenge, aliiomba mamlaka kupanga bei elekezi kulingana na umbali halisi wa maeneo inakopaswa kufika kwani maeneo mengi ya mkoa huo yako mbali na makao makuu ya wilaya ili waone faida ya kufanya biashara hiyo na wakulima wafikishiwe bidhaa hiyo karibu na maeneo yao.

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**BERNADETA MARMO FISSO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 585 CMD** aina ya **SUZUKI CARRY.** Chassis namba **DD51T375930.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/72098/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**JOSEPH MWASI MASINI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 524 CKM** aina ya **TOYOTA HARRIER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/2278/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA**

**KITUO CHA KARABAGAINE**

**SHAURI LA MADAI NO. 24/2024**

**MAHAMUDU RASHID..........................MDAI**

**DHIDI YA**

**OBADIA PIUS MUSSA ..................MDAIWA**

OBADIA PIUS MUSSA unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 07/05/2024 saa 08:30 hrs asubuhi kuja kujibu madai ukiwa na mashahidi wako.

Kwa kuwa ni siku ya kukata shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hili na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 24/04/2024.

C. R. RICHARD
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE.

## KUPOTEA KWA CHETI



**NAOMI WAMBURA GIKARO,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba za usajili **IRDP/BDU/20/000083,** Kilichotolewa na chuo cha **MIPANGO DODOMA Mwaka 2023.** Yeyote atakaekiona atoe taalifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/66574/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**PAUL CASTOR MWASHILILI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 559345,** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO tarehe 13 February 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/70602/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**RITTA NYENDO MAGERO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 579 CJU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/5438/2023.**

HEAD OFFICE
Makumbusho Business Complex
P.O.BOX. 21566,
Dar es Salaam-Tanzania

SoftFinance.

Mobile. +255(0)717 718 519
+255(0) 22 270 1320
Email : mkopo@softfinance.co.tz
Web : www.softfinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

SOFT FINANCE LTD INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ILIYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| S\N | MKOPAJI/MDHAMINI | DHAMANA | UMILIKI NA ENEO LA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWANTUMU MOHAMED. HAMISI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MIVUMONI | J & J RECOVERIES | 14-05-2024 |
| 2 | JACQULINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – TUANGOMA | LEGENDS AUCTION MART | 07-05-2024 |
| 3 | IBRAHIM IDDI KONDO | KIWANJA | MKATABA WA MAUZIANO – KISOPWA | KAZI WORK INTERPRISES | 14-05-2024 |
| 4 | YUSUPH ISSA BITAMALE | KIWANJA | MKATABA WA MAUZIANO – KIGAMBONI | LEGENDS AUCTION MART | 14-05-2024 |
| 5 | GLORIA DAMASI MRINDA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA STOP OVER | LEGENDS AUCTION MART | 14-05-2024 |
| 6 | MOHAMED ABDALLAH ATHUMANI | KIWANJA | MKATABA WA MAUZIANO – LANGWENI | KAZI WORK INTERPRISES | 14-05-2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

## TANGAZO

**MASAHIHISHO YA TANGAZO LILILOKOSEWA LA TOLEO LA TAREHE 25 APRILI 2024 KWENYE GAZETI LA NIPASHE**

KCBL Together, Transforming Lives

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED (KCBL)

## PUBLICATION OF AUDITED FINANCIAL STATEMENTS

### Issued pursuant to regulations 7 and 8 of the Banking and Financial Instituions (Disclosures) Regulation, 2014

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2023 | Previous Year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 153,897 | 122,302 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 593,293 | 480,936 |
| 3 | Balances with other banks and financial institutions | 1,477,957 | 662,153 |
| 4 | Investments in Government securities | 4,708,764 | - |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | 7,304,528 | 2,095,949 |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probable losses) | 8,762,374 | 7,493,647 |
| 12 | Other assets | 161,385 | 337,138 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 2,659,042 | 366,706 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **25,821,239** | **11,558,831** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 9,327,709 | 5,923,744 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | - | - |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | - | - |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 185,949 | 1,233,997 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **9,513,658** | **7,157,741** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **16,307,581** | **4,401,090** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 24,987,034 | 15,305,153 |
| 32 | Capital reserves | 88,892 | (65,457) |
| 33 | Retained earnings | (10,992,955) | (11,165,866) |
| 34 | Profit (Loss) account | 423,348 | 327,260 |
| 35 | Other capital accounts | 1,801,262 | - |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **16,307,581** | **4,401,090** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 301,674 | 166,808 |
| 40 | Allowances for probable losses | 83,916 | 72,945 |
| 41 | Other non performing assets | | |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | 63.16% | 38.08% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 3.41% | 2.20% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 94.84% | 127.73% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 33.93% | 64.83% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 34.15% | 65.05% |
| (vi) | Deposits Growth | 57.46% | 3.97% |
| (vii) | Assets growth | 123.39% | 44.01% |

### STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2023 | Previous Year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 1,629,543 | 937,564 |
| 2 | Interest Expense | 139,612 | 47,025 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **1,489,931** | **890,539** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | 10,971 | (1,787) |
| **6** | **Non Interest Income:** | **325,643** | **694,658** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 308,087 | 309,531 |
| | 6.3 Dividend Income | | |
| | 6.4 Other Operating Income | 17,556 | 385,127 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **1,345,240** | **1,217,369** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 528,764 | 503,285 |
| | 7.2 Fees and Commission | 665,274 | 609,087 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 151,202 | 104,997 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **459,363** | **369,615** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **36,015** | **42,355** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **423,348** | **327,260** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | **1,787,070** | **-** |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | **2,210,418** | **327,260** |
| 13 | Number of Employees | 24 | 23 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | 0 | 0 |
| 15 | Number of Branches | 1 | 1 |
| | **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | 1.64% | 2.83% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | 2.60% | 7.44% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 69.36% | 74.47% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | 16.84% | 11.77% |

### STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current year 31st Dec 2023 | Previous year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| I: | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income (Loss) | 459,363 | 369,615 |
| | **Adjustments for:** | | |
| | - Impairment/Amortization | 63,850 | 38,753 |
| | - Prior Year Adjustment | | - |
| | - Depreciation | 85,169 | 66,246 |
| | - Net change in Loans and Advances | (1,268,727) | (2,855,662) |
| | - Gain/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | 3,403,965 | 496,480 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | - | - |
| | - Net change in Other Liabilities | (1,048,048) | 956,091 |
| | - Net change in Other Assets | 169,739 | (255,247) |
| | - Tax Paid | (30,000) | (93,119) |
| | - Others (specify) | (198,346) | 186,287 |
| | - Due to other banks | (3,677,357) | (89,406) |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(2,040,392)** | **(1,179,962)** |
| II: | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purchase of Fixed Assets | (593,583) | (8,143) |
| | T Bills | (200,375) | - |
| | T Bonds | (6,008,389) | - |
| | Investment | (31,222) | - |
| | Others (Adjustment on Property Plant and Equipment) | (46,510) | (15,414) |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | **(6,880,079)** | **(23,557)** |
| III: | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Preference share | 7,000,000 | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 2,681,881 | 1,326,163 |
| | Change in Reserve | | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others (Adjustment in retained earnings) | | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Activities*** | **9,681,881** | **1,326,163** |
| IV: | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **761,410** | **122,644** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **909,966** | **787,322** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **1,671,376** | **909,966** |

Godfrey J. Ng'urah
**GENERAL MANAGER** 4/24/24

Kinyaki O. Kinyaki
**HEAD OF FINANCE AND ADMINISTRATION** 4/24/24

Apolinary S. Kityamwi
**HEAD OF INTERNAL AUDIT** 4/24/24

The above extracts are from the financial statements of the Bank for the year ended 31st December,2023 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards (IFRS).The financial statements were audited by INNOVEX AUDITORS and received a unqualified report.The financial statements were approved by the Board of Directors on 24th April, 2024 and signed on their behalf by:

| Name | Signature | Date |
|---|---|---|
| 1. Prof. GERVAS M. MACHIMU, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS | | 4/24/24 |
| 2. CPA. MWAMINI J. MUSSA, DIRECTOR | | 4/24/24 |

### CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2023
(Amounts in '000' shillings)

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at 1st January, 2023** | **15,305,153** | **-** | **(10,969,520)** | **65,457** | **-** | **4,401,090** |
| Profit for the year | | - | 423,348 | - | - | **423,348** |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | **0** |
| Transactions with owners | 9,681,881 | - | - | - | - | **9,681,881** |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | **0** |
| Regulatory Reserve | - | - | (23,435) | 23,435 | - | **0** |
| General Provision Reserve | - | - | | | | **0** |
| Others(Adjustment) | - | - | - | - | | **0** |
| **Balance as at 31st December, 2023** | **24,987,034** | **-** | **(10,569,607)** | **88,892** | **-** | **14,506,319** |
| | | | | | | |
| **Balance as at 1st January, 2022** | **13,978,990** | **-** | **(11,257,904)** | **26,581** | **-** | **2,747,667** |
| Profit for the year | | - | 327,260 | - | - | 327,260 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 1,326,163 | - | - | - | - | 1,326,163 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | 92,038 | (92,038) | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | | - |
| **Balance as at 31st December, 2022** | 15,305,153 | - | (10,838,606) | (65,457) | - | 4,401,090 |
| **Prior Year Adjustment** | - | - | (130,914) | 130,914 | | - |
| **Restated Balance as at 31st December, 2022** | **15,305,153** | **-** | **(10,969,520)** | **65,457** | **-** | **4,401,090** |

# Z'BAR YANG'ARA RIADHA EAAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Taifa ya Riadha ya Zanzibar imeshika nafasi ya kwanza kwenye mashindano ya Riadha ya Afrika Mashariki na Kati (EAAR), kwa vijana walio chini ya miaka 18 wakati Kenya wakishika nafasi hiyo kwa timu ya chini ya umri wa miaka 20, katika mashindano hayo yaliyokuwa yakifanyika Zanzibar Ijumaa na Jumamosi iliyopita.

Zanzibar imefanikiwa kushika nafasi hiyo baada ya kujinyakulia medali sita za dhahabu, za fedha tano na ya shaba moja na kufanya idadi medali kuwa 12.

Mashindano hayo ambayo yalifanyika katika Uwanja wa New Amaan Complex, yalishirikisha nchi saba lakini kwa upande wa U-18 zilishiriki sita, ambapo Kenya ilishika nafasi ya pili.

**Kenya imeondoka na medali tano za dhahabu tatu za fedha na nne za shaba wakati Uganda imeibuka mshindi wa tatu baada ya kuvuna medali saba zikiwamo tatu za dhahabu, fedha tatu na moja ya shaba.**

Kwa upande wa Tanzania Bara, wao walishika nafasi ya nne baada ya kujinyakulia medali nane zikiwemo mbili za fedha na sita za shaba.

Katika mashindano hayo, Djibouti imeshika nafasi ya tano baada ya kujinyakulia medali mbili moja ya fedha na moja ya shaba, wakati Sudan Kusini imeshika nafasi ya sita ambayo ni ya mwisho ikiondoka patupu bila medali yoyote.

Kwa upande wa U-20 Kenya ambao walishika nafasi ya kwanza waliibuka na medali 10, sita za dhahabu, mbili za fedha na mbili za shaba, wakati Uganda ilishika nafasi ya pili wakiwa na medali saba, nne za dhahabu, mbili za fedha na moja ya shaba.

Zanzibar katika umri huo mameshika nafasi ya tatu wakiwa na medali tatu za dhahabu, tatu za fedha na nne za shaba, wakati Tanzania imeshika nafasi ya nne wakiwa na medali moja ya dhahabu, fedha tatu na tatu za shaba.

Nafasi ya tano imekwenda kwa Sudan Kusini iliyobeba medali mbili, moja fedha na moja ya shaba na Djbouti ikishika nafasi ya sita baada ya kuondoka na medali moja ya fedha moja na shaba moja.

Zanzibar ambayo ilikuwa wenyeji wa michuano hiyo, pia imefanya vizuri katika michezo midogo midogo ikiwamo kurusha tufe, mkuki, kisahani.

# *Wema rasmi sasa Kisura wa Royco*

**Na Imani Nathaniel**

MUIGIZAJI maarufu wa Filamu nchini na Mtangazaji wa Kipindi cha 'Cook with Wema Sepetu', Wema Sepetu, rasmi ametangazwa kuwa Kisura wa Royco.

Wema alikwaa nafasi hiyo, baada ya kutangazwa juzi jijini Dar es Salaam katika hafula ya uzinduzi wa 'Jilambe na Royco Sotojo Maharage'.

Akizungumzia kuhusu nafasi hiyo, Wema lisema: "Najihisi mwenye bahati kwani nimekuwa miongoni mwa wanafamilia wa kiungo cha Royco, nimeanza kuwa kisura wao mtaniona sana.

"Najisikia faraja kwa kuwa mapishi ni kitu kipo kwenye damu yangu na ndio kitu napenda, hivyo basi kuwa Kisura wa Royco kwangu ni fahari na hawatajutia mimi kuwa mwanafamilia wao," alisema Wema wakati akielezea furaha yake ya kuwa kisuru wa kiungo hicho cha chakula.

Kwa upande wa Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Flora Mgonja, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliipongeza Kampuni ya Unilever kwa jitihada kubwa wanazofanya kwa kuunga mkono juhudi za Rais Samia kuhakikisha Watanzania wanapata milo iliyo bora kwa kutumia bidhaa ya Royco ambayo ni kiungo unachoweza kutumia katika mboga husasan Maharage.

Aliongeza kuwa serikali itaiunga mkono na kuiwezesha kampuni hiyo kupata masoko ili kuwezesha Watanzania kupata ajira katika kujikwamua na umasikini kwa maana hiyo ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Unilever Afrika, Luck Ochieig, aliwaomba Watanzania waipokee bidhaa hiyo ambayo itapatikana sokoni kila mahali kwani ni rahisi ambayo itawafaa kwa matumizi bora ya mboga na kuongeza ladha ya chakula.



Mchezajj wa timu ya DSM Soccoer Academy, Said Maneno, akijaribu kumtoka mchezaji wa timu ya JMK walipokutana katika mchezo wa kirafiki uliopigwa kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yawataka Waogeleaji kuwika kuwania kufuzu Olimpiki

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limewataka waogeleaji wa timu ya taifa kuhakikisha wanafanya vema kwenye mashindano ya Kuogelea ya Afrika (Africa (Aquatics Swimming Championships), yatakayoanza kesho hadi Mei 2, mwaka huu, nchini Angola yakiwa na lengo la kuwania kufuzu michuano ya Olimpiki baadaye nchini Ufaransa.

Akizungumza jana wakati akikabidhi Bendera ya Taifa kwa timu hiyo, Ofisa Michezo wa BMT, Charles Maguzu, ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji, Neema Msitha, alisema anaamini waogeleaji hao watafanya vizuri kutokana na ubora waliokuwa nao.

"Mnakwenda kuiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo, nendeni mkapambane kuhakikisha mnashinda, mnaipeperusha bendera ya taifa letu kwa kupata medali za ushindi Watanzania tupo nyuma yenu," alisema Maguzu.

Aidha, aliwapongeza kwa kupata nafasi adimu ya kuteuliwa kwenye timu ya taifa kwenda kuiwakilisha nchi huku pia akiipongeza Kamati ya Utendaji ya Chama cha mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), kwa juhudi inayofanya kuinua vipaji vya vijana kupitia mchezo huo ambao kwa sasa unazidi kushika kasi.

"Ninaipongeza Kamati ya Utendaji kwa kutoa fursa kwa makocha wenu kwenda nje ya nchi kunapotokea mashindano ya Kimataifa ili kila mmoja akaonyeshe uwezo wake tofauti na vyama vingine vimekuwa vikitoa fursa kwa mtu mmoja jambo ambalo linavunja moyo," alisema.

Kwa upande wa Rais wa Chama hicho, David Mwasyoge, naye aliwapongeza waogeleaji hao kutokana na ubora wanaozidi kuuonyesha katika mashindano mbalimbali ambayo wamekuwa wakishiriki na kuweka wazi kuwa wamefanya kazi kubwa mpaka kufika walipo sasa.

Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Yusuph Isiki, alisema ameandaa waogeleaji wake vizuri akiwa na matumaini ya kwenda kupata matokeo mazuri.

Wakati huo huo nahodha wa timu hiyo, Sophia Latiff, ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, alisema malengo yao ni kwenda kuvunja rekodi zao ili waweze kupunguza muda licha ya kwamba wanatarajia kupata upinzani mkubwa.

Tanzania inawakilishwa na Sophia Latiff, Collins Saliboko pamoja na Hilal Hilal.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WALKER AWANIWA BAYERN

Bayern Munich wanapanga uhamisho mwingine wa kumnunua mlinzi wa Manchester City, Kyle Walker, baada ya kushindwa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Star)***

### RATCLIFFE, MENDES WAKUTANA

MMILIKI mwenza wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, amekutana na wakala, Jorge Mendes, ambaye wateja wake ni pamoja na mmoja wa walengwa wa klabu hiyo katika kiungo wa kati wa Benfica na Ureno, Joao Neves, 19. ***(Mirror)***

### LACROIX AWANIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace iko tayari kujiunga na mbio za kumsajili beki wa kati wa Wolfsburg, Maxence Lacroix mwenye umri wa miaka 24, katika msimu huu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### SLOT ATAJWA LIVERPOOL

ARNE Slot atateuliwa kuwa kocha mkuu wa Liverpool baada ya mabadiliko ya muundo wa klabu. ***(Times)***

### LOPETEGUI NA WEST HAM

MATUMAINI ya West Ham ya kumteua kocha wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui, kuchukua nafasi ya David Moyes kama kocha msimu huu yanaonekana kukamilika huku AC Milan wakikaribia kuafikiana. ***(Guardian)***

### RODRIGUEZ KUTUA BARCA

BARCELONA inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 30, kutoka klabu nyingine ya LaLiga ya Real Betis. ***(Sport)***

### CUBARSI MKATABA MPYA

BARCELONA inapanga kulinda mustakabali wa mlinzi wa kati Pau Cubarsi mwenye umri wa miaka 17, baada ya kupendekeza mkataba mpya kwa Mhispania huyo ambao unajumuisha kipengele cha kutolewa cha euro milioni 500. ***(AS)***

### BURUNO ATETEWA UNITED

KIUNGO wa zamani wa Manchester United na Hispania, Juan Mata mwenye umri wa miaka 35, anaamini kuwa klabu yake hiyo ya zamani inapaswa kujenga timu yoyote ya baadaye karibu na Bruno Fernandes wa Ureno mwenye umri wa miaka 29. ***(ESPN)***

### KARIUS KUONDOKA NEWCASTLE

GOLIKIPA wa Ujerumani, Loris Karius mwenye umri wa miaka 30, ataondoka Newcastle United kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### CHIESA KUFUNGWA JUVE

KLABU ya Juventus inashughulikia kuongeza mikataba ya washambuliaji wa Italia, Federico Chiesa, 26 na Mserbia Dusan Vlahovic, 24. ***(Rudy Galetti)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: KUTAWAKA MOTO NIKIZUNGUMZA KWA SASA

**Ni baada ya kuzozana na Klopp wakitoka sare na West Ham, wakati akitaka...**

**LONDON,** England

MAHAMED Salah amekataa kufichua sababu za kubwatukiana na kocha wake, Jurgen Klopp, wakati Liverpool ilipotoka sare ya mabao 2-2 na West Ham kwenye Uwanja wa London Jumamosi, akisema: "Kutakuwa moto nikizungumza."

**Klopp na Salah walionekana kutoleana maneno huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri akisubiri kuingia uwanjani akitokea benchi zikiwa zimesalia dakika 13, wakati wachezaji wengine wa akiba Darwin Nunez na Joe Gomez wakiingilia kati ili kutuliza hali hiyo.**

Salah alikataa fursa ya kuzungumza na waandishi wa habari baada ya filimbi ya mwisho ya mchezo huo kule London Mashariki, akisema: "Kutakuwa moto nikizungumza."

Sare hiyo ililetea pigo zaidi kwa matumaini ya Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, huku timu hiyo ya Klopp sasa ikiwa pointi mbili nyuma ya Arsenal, ambayo inaweza kuendeleza uongozi wao kileleni mwa msimamo ambapo jana Jumapili ilikuwa ikicheza na Tottenham Hotspur.

Hapo awali Klopp alikataa kueleza sababu za kutoelewana.

"Tulizungumza juu ya hilo kwenye chumba cha kubadilishia nguo na imefanywa kwangu, ni hivyo tu," alisema bosi huyo wa Liverpool.

Mkataba wa Salah pale Anfield unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Mnamo Februari, vyanzo vilimwambia Rob Dawson wa ESPN kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alikuwa mmoja wa nyota kadhaa wa Ligi Kuu England ambao watalengwa na Klabu za Saudi Pro League katika dirisha la uhamisho la majira ya joto.

Liverpool itamenyana na Tottenham Jumapili ijayo kwenye Ligi Kuu ikiwa ni mechi ya kwanza kati ya tatu zilizosalia msimu huu, wakati ambapo wanaweza kuwa na pointi nane nyuma ya Arsenal ikiwa vinara hao wa ligi hiyo watashinda michezo yao miwili ijayo kati ya minne ya mwisho.

## HABARI MICHEZO

# SOLSKJAER KATIKA MAZUNGUMZO KUINOA CANADA



**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ni miongoni mwa majina yanayoripotiwa kuwa katika orodha ya kuwania kuwa Kocha Mkuu wa Canada wakati kwa Kombe la Dunia la FIFA la 2026.

Solskjaer amekuwa hana kazi tangu aondoke Old Trafford mwaka 2021.

Gazeti la Evening Standard limeripoti kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 51, amewasiliana na Chama cha Soka cha Canada kuhusu kazi iliyo wazi ya kuiongoza timu yao ya Taifa ya Wanaume.

Solskjaer hajawahi kufanya kazi katika soka la kimataifa, ingawa kwa chini ya umakini kwamba usimamizi wa klabu unaweza kuvutia.

Wote wawili, Jose Mourinho na Frank Lampard wanasemekana kukataa nafasi hiyo, lakini Jesse Marsch alitafutwa pamoja na Aitor Karanka na Paul Clement.

Kuna maoni kwamba kuwaniwa kwa Clement kunaweza kuwa njama ya hatimaye kumpata Carlo Ancelotti, ambaye amekuwa na ukaribu na kocha huyo wa England tangu walipokuwa pamoja Chelsea miaka 15 iliyopita.

Bobby Smyrniotis, Kocha Mkuu wa Klabu ya Forge FC ya Ligi Kuu ya Canada, ni mgombea mwingine na tayari anaaminika kuwa amehojiwa kama chaguo bora zaidi la ndani.

Canada itakuwa mwenyeji wa Kombe lijalo la Dunia kwa pamoja na Marekani na Mexico, huku michezo kwenye michuano hiyo ikichezwa katika mji wa Vancouver na Toronto.

# Magalhaes mkataba mpya Arsenal




**LONDON,** England

ARSENAL imeanza mazungumzo na Gabriel Magalhaes kuhusu mkataba mpya na ulioboreshwa, kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa patina mzuri na William Saliba katikati mwa safu ya ulinzi ya Arsenal, na kuisaidia klabu hiyo kuuwinda ubingwa kwa msimu wa pili mfululizo.

'Washikabunduki' hao kwa sasa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu mbele ya Manchester City kabla ya mechi za jana Jumapili.

Liverpool pia wako kwenye kinyang'anyiro hicho, lakini waliona matumaini yao yamefifia baada ya kipigo cha 2-0 kutoka kwa wapinzani wa Merseyside Everton Jumatano na sare na West Ham Jumamosi.

Gabriel tayari ana mkataba wa kuendelea kuitumikia Arsenal hadi 2027, lakini Evening Standard limeripoti kwamba mazungumzo yanaendelea na wawakilishi wa mchezaji huyo kuhusu suala la kuboreshwa kwa mkataba mpya.

Mbrazil huyo amecheza mechi 46 katika mashindano yote msimu wa 2023/24 - akiimarisha nafasi yake pamoja na Saliba, ambaye amefurahia kampeni ya kuvutia.

Aliwasili Septemba 2020 kutoka Lille kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 27, na alisaini mkataba mpya wa miaka mitano na miaka miwili baadaye baada ya kuwa kiungo mkuu wa kikosi cha Arteta.

Iwapo Gabriel atapata mkataba mpya, atafuata nyayo za Saliba, ambaye alitia saini mkataba mpya Julai mwaka jana akiweka mustakabali wake Arsenal hadi 2028, na Ben White, ambaye amepata uhakika mkubwa kutokana na kiwango chake cha beki wa kulia.

White aliweka mustakabali wake Arsenal kwa miaka mingine minne Machi, huku kiwango chake cha kuvutia kilisababisha wito wa Gareth Southgate kumrejesha kwenye kikosi cha England kwa mara ya kwanza tangu arejee nyumbani mapema kutoka Kombe la Dunia la 2022.

# Wachezaji wana imani na Pochettino

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Chelsea bado wanamuunga mkono kocha wao mkuu, Mauricio Pochettino licha ya matatizo yao msimu huu, kwa mujibu wa ripoti.

'The Blues' hao wanaweza kumaliza msimu wakiwa nje ya katika nafasi ya kufuzu Ligi ya Europa mwaka wa pili mfululizo, na hivi Jumanne walidhalilishwa kwa mabao 5-0 na wapinzani wao Arsenal, huku Jumamosi wakitoka sare ya 2-2 na Aston Villa.

Shinikizo linaongezeka kwa Pochettino, kocha huyo mwenye umri wa miaka 52, bado anaheshimiwa sana na wengi wa chumba cha kubadilishia nguo, huku Standard ikiripoti kuwa wachezaji wanamuunga mkono.

Nhodha Reece James na msaidizi wake, Ben Chilwell, wameshindwa kutoa ushawishi na usaidizi mwingi kama wao au Pochettino walivyotarajia kutokana na majeraha.

Baadhi ya wajumbe wa bodi wanaamini Pochettino anastahili kuendelea na nafasi yake kuelekea msimu ujao, kwani wanatambua changamoto alizokabiliana nazo na kupongeza juhudi zake za kuvuka mazingira magumu.

Muargentina huyo alisaini mkataba wa miaka miwili na Chelsea msimu uliopita wa majira ya joto ambao ulijumuisha chaguo la miezi 12 zaidi.

Na kuanzia sasa hadi mwisho wa msimu huu, Pochettino atakuwa akitumia kila juhudi kudumisha nafasi yake katika kiti cha moto huko London Magharibi.

Anabakia na imani kwamba mbinu zake hatimaye zitaleta majibu kama ilivyokuwa wakati akiwa na kikosi cha vijana cha Tottenham Hotspur.



HABARI MICHEZO

## Gamondi aanza

INATOKA UKURASA 24

kupewa kadi nyekundu, hali ambayo wapinzani wao hao walitumia nafasi hiyo kupata bao moja.

"Sio mchezo nzuri kwangu kwa sababu tumepoteza, ninaimani tungekuwa kamili wasingetufunga, kipindi cha kwanza tukiwa 11 kwa 11 hawakupatanafasi ya kufunga hadi dakika 69 tulienda 0-0 baada ya kadi nyukundu ndio wakatufunga," alisema Ouma.

Aliongeza kuwa mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa timu zote mbili na anawapongeza wachezaji wake kufanya kile alichokielekeza kwenye uwanja wa mazoezi na kuhamisha uwanjani.

## Benchikha atoa sababu kuvunja

INATOKA UKURASA 24

"Kiukweli tumefurahishwa na matokeo ya leo, na tumecheza leo kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wetu, yaani tumecheza kwa ajili ya mashabiki wenye Simba yao, na ubingwa huu ni wao, tunawaambia kuwa bado tunaweza, tunapambania furaha yao na kwa ajili ya nembo ya klabu.

Tunarudi kwenye ligi, kikubwa baada ya kombe hili, nadhani mashabiki watakuwa na imani na sisi, watarejea kwa wingi viwanjani ili kutupa sapoti, wasituache, sisi ndiyo wachezaji wao mpaka mwisho wa msimu, tumejipanga vizuri tutahakikisha mechi zote zilizobaki tunashinda," alisema Kibu Denis.

Kiungo mkabaji, Mzamiru Yassin alisema wao kama wachezaji walicheza kwa ajili ya kulitwaa kombe hilo ili kurudisha imani kwa mashabiki na kweli wamefanya hivyo, huku akiwaangukia kuwa ubingwa huo sasa uwafanye waje viwanjani kuwapa sapoti kama zamani na wao watahakikisha kuwa wanawapa furaha.

Kwa upande wa Saido Ntibazonkiza yeye aliwashukuru mashabiki waliojazana uwanjani kuwashangilia, akisema shabiki wa kweli hawezi kuiacha timu yake

"Huu ni mpira, shabiki wa kweli hawezi kuiacha timu yake, hawa waliopo hapa wanaotushangilia na wanaoendelea kutupa sapoti ndiyo mashabiki wa kweli, katika soka huwezi kushinda kila siku, hata timu kubwa huwa zinapoteza," alisema.

Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala', alisema ubingwa walioupata ni chachu ya kufanya vema kwenye mechi zilizosalia za Ligi Kuu.

Ushindi huo unaifanya Simba kuwa bingwa wa kombe hilo mara sita sawa na Yanga, ambapo kwa sasa zote zinaongoza kwa kutwaa mara nyingi zaidi.

Simba ilifanya hivyo mwaka 1993, 1994, 1995, 2001 na 2002, kabla ya kutwaa tena juzi, huku Yanga ikilichukua 1983, 1987, 1991, 1996, 1997 na 2000.

# NBC YATAMBUA MCHANGO WA POLISI ULINZI MATUKIO YA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu, Kilimanjaro**

BENKI ya NBC imekabidhi msaada wa vitanda 28 kwa Shule ya Polisi Tanzania (TPS), iliyopo Moshi mkoani Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya utambuzi wa jitihada za jeshi hilo katika kusimamia ulinzi na usalama kwenye matukio mbalimbali ya michezo yanayodhaminiwa na benki hiyo ikiwamo Ligi Kuu ya soka Tanzani ya NBC (NBC Premier League).

**Matukio mengine ni pamoja na Ligi Daraja la Kwanza (NBC Championship), Ligi ya Vijana (NBC Youth League) pamoja na mbio za NBC Marathon zinazoandaliwa na benki hiyo na kufanyika kila mwaka jijini Dodoma.**

Hafla fupi ya makabidhiano ya vitanda hivyo ilifanyika jana shuleni hapo ambapo ilishuhudiwa Meneja wa NBC Tawi la Moshi, Lazaro Mollel, akimkabidhi Mkuu wa Shule hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, SACP Ramadhani Mungi, msaada huo kwa niaba ya benki hiyo.

Mollel alisema pamoja na kutambua jitihada za jeshi hili katika kuimarisha ulinzi na usalama kwa jamii yakiwamo matawi ya benki hiyo na wateja wake, ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili pia unaonekana kwenye usimamizi wa ulinzi na usalama wakati wa mechi za mpira wa miguu kwenye matukio hayo ya kimichezo hali ambayo imekuwa ikiongeza mvuto kwa mashabiki na washiriki wa matukio hayo na hivyo kuisaidia benki hiyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika udhamini wa matukio hayo.

"Jeshi la Polisi ni miongoni mwa wadau wakubwa wa Benki ya NBC hapa nchini. Uhusiano mkubwa uliopo baina ya taasisi hizi mbili unatokana na kutegemeana baina yetu kutokana na majukumu yetu ambapo kupitia huduma zetu za kibenki Jeshi la Polisi limekuwa likinufaika kupitia huduma za vipaumbele kwao na sisi pia kama benki tumekuwa tukinufaika na huduma za jeshi hili muhimu hususan kwenye suala zima la kuhakikisha ulinzi na usalama katika matukio yetu ya kimichezo na ulinzi wa rasilimali zetu wakiwapo wafanyakazi, fedha na majengo bila kusahau usalama wateja wetu pia," alibainisha.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, SACP Mungi, pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa kutambua mchango wao kwenye matukio hayo ya kimichezo na ulinzi wa rasilimali zake, alisema shule hiyo itaendelea kuzalisha askari wenye weledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yao kisasa yakiwamo yale ya kimichezo.

Hata hivyo, alibainisha kuwa shule hiyo inahitaji misaada mingi ya namna hiyo kutokana na ongezeko la wanafunzi ambao kwa sasa wapo takriban 5,000.

"Wakati shule imehamishiwa hapa Moshi mwaka 1954, ilikuwa na wanafunzi 600 ila kwa sasa wapo takriban 5,000. Ongezeko hili linakwenda sambamba na la mahitaji muhimu ikiwamo mazingira bora ya kuishi na kupumzika kwa wanafunzi. Mazingira bora ya kufundishia yaani madarasa na vifaa bora vya kufundishia, serikali imekuwa ikijitajidi kufanikisha haya yote ila bado tunahitaji jamii pia ione umuhimu wa kuisadia kwenye hili na hiyo ndio sababu tunawashukuru sana NBC kwa msaada huu," alisema.

Akizungumzia msaada huo SACP Mungi alisema utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uhaba wa vitanda shuleni hapo na hivyo kuwawezesha wanafunzi hao kuendelea na masomo yao wakiwa katika mazingira bora ya kupumzikia.




Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Moshi, Lazaro Mollel (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania (TPS), Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, SACP Ramadhani Mungi, msaada wa vitanda 28 kutoka benki hiyo ikiwa ni sehemu ya utambuzi wa jitihada za jeshi hilo katika kusimamia ulinzi na usalama kwenye matukio mbalimbali ya michezo yanadhaminiwa na benki hiyo, sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama kwa jamii yakiwamo matawi ya benki hiyo na wateja wake. Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika mwishoni mwa wiki shuleni hapo, Moshi mkoani Kilimanjaro. **MPIGAPICHA WETU**

# Malindi, Mlandege FC dimbani Dabi ya Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MIAMBA ya soka Zanzibar, Malindi SC na Mlandege FC, inatarajiwa kushuka dimbani leo kwenye mchezo wa 'Dabi' ya Zanzibar Ligi Kuu mzunguko wa 21 wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Timu hizo kongwe katika medali za soka Visiwani Zanzibar, zitapepetana leo katika Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri huku zote zikiwa bado zinasaka alama za kujihakikisha zinabaki Ligi Kuu mwishoni mwa msimu, Mlandege FC wakiwa nafasi ya 10, wakati Malindi SC wakiwa nafasi ya tisa timu na kila moja ikiwa na pointi 25.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Malindi SC, Suleiman Mohmed, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa timu zote bado zinahitaji alama za kujihakikishia kubaki Ligi Kuu.

Alisema hawakuwa na mwanzo mzuri wa kwenye ligi kwa upande wao na hata kwa wapinzani wao, hivyo lazima kila mmoja atakuja na mbinu mbadala za kusaka ushindi.

Alisema katika mchezo huo wanahitaji alama tatu na zitapatikana iwapo wachezaji watacheza kwa utulivu na kutokuwa na hofu ya mchezo.

"Mchezo huu unahitaji uzoefu kwa wachezaji na hata makocha hasa katika kufanya maamuzi ya haraka uwanjani, hatuhitaji kutumia nguvu nyingi bali wachezaji wawe na uwezo wa kuwasoma wapinzani wetu," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Mlandege FC, Hassan Ramadhani, alisema amewaandaa wachezaji wake vizuri kuhakikisha wanacheza kwa ushindani katika mchezo huo muhimu.

Alisema bado kikosi chake kipo imara na kina hamasa kubwa kuona wanashinda mchezo huo dhidi ya wakongwe wa soka na dabi ya miaka mingi.

Ramadhani alisema mchezo wa dabi siku zote huwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, hivyo wao Mlandege FC wamejipanga kuwakabili wapinzani wao.

"Tunaenda uwanjani kupambana kuhakikisha tunapata alama ambazo zitatufanya tupate matokeo mazuri katika michezo yetu hii iliyobaki," alisema.

# Michezo

Jumatatu Aprili 29, 2024

Nipashe




Wachezaji wana imani na Pochettino UKURASA 22

## WAONDOKA KAMA WALIVYOKUJA...!




Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, Kamal Boujnane na Farid Zemit, katika picha wakati wakitambulishwa walipojiunga na klabu hiyo kabla ya jana kuachana na klabu hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Benchikha atoa sababu kuvunja mkataba Simba

## Aondoka na wasaidizi wake wawili, wachezaji Msimbazi nao sasa waapa...

**Saada Akida na Adam Fungamwangwo**

HATIMAYE ni rasmi sasa Klabu ya Simba, imefikia makubaliano ya pande zote mbili ya kuvunja mkataba kati yake na Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha pamoja na wasaidizi wake wawili Kamal Boujnane na Farid Zemit.

**Awali, baada ya kutwaa Kombe la Muungano juzi visiwani Zanzibar kwa kuifunga Azam FC bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa New Amaan Complex, zilizuka taarifa za chini kwa chini kuwa kocha huyo ameomba kuvunja mkataba kutokana na kile kilichodaiwa kuwa haioni Simba ikimfanya kupata mafanikio ya kutwaa makombe makubwa barani Afrika.**

Simba ilishindwa kufuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa chini yake, kisha kutolewa kwenye Kombe la FA maarufu CRDB Bank Confederation Cup huku pia ikiwa na nafasi finyu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, mataji hayo mawili ndiyo yanayotoa nafasi kwa klabu kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Taarifa zaidi zilidai kuwa Benchikha anamini kuwa Simba haina wachezaji bora ambao wanaweza kutimiza ndoto zake hizo.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema Mwalimu Benchikha ameomba kuvunja mkataba wake kutokana na matatizo ya kifamilia yanayomkabili nyumbani kwao Algeria.

Alisema Benchikha ameueleza uongozi wa Simba kuwa anauguliwa na mkewe, hivyo anahitaji muda kuwa karibu naye na kumuuguza, kwa namna hiyo kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hilo uongozi umeridhia ombi la kocha huyo.

"Uongozi wa Klabu ya Simba unamshukuru Mwalimu Abdelhak Benchikha kwa kipindi chote alichotumia ndani ya timu yetu na tunamtakia kila la heri na tunamuombea mkewe apate afya njema," alisema Ahmed.

Wakati huo huo, uongozi wa klabu hiyo umemteua Mwalimu Juma Mgunda kukiongoza kikosi hicho akisaidiwa na Selemani Matola hadi hapo Bodi ya Wakurugenzi itakapotoa uamuzi mwingine.

Mwalimu Juma Mgunda ataanza kazi katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC dhidi ya Namungo FC utakaochezwa kesho, Jumanne Ruangwa Mkaoni Lindi katika Uwanja wa Majaliwa saa 12 jioni.

Katika hatua nyingine, baada ya Simba kutwaa ubingwa wa Muungano, wachezaji wa timu hiyo wamesema wameamua kuutoa kwa mashabiki wao, wakisema utakuwa chachu ili baadhi yao waliokata tamaa warejee kuwasapoti, huku wao wakiendelea kupigania nembo ya klabu hiyo.

Wakizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya fainali ya Muungano, Uwanja wa New Amani Complex, Zanzibar, juzi, Simba ikipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, likiwekwa wavuni na kiungo mkabaji raia wa Senegal, Babacar Sarr, wachezaji hao wamesema ubingwa walioupata unakwenda kwa mashabiki wao ambao siku za karibuni wamekuwa hawana furaha kutokana na timu yao kutofanya vema, huku wakiwataka sasa kurejea na kujaza viwanja kama ilivyokuwa zamani.

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi aanza kuuona ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, wachezaji wake wamekuwa wakipambana uwanjani kusaka pointi kwa dakika zote kwa ajili ya kufikia malengo yao, jambo ambalo linampa matumaini makubwa ya kutetea ubingwa wao, lakini hawajawa na uhakika kwa asilimia 100.

Yanga juzi waliendelea kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutetea ubingwa wao baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kufikisha pointi 64 kileleni, bao hilo pekee likifungwa na Joseph Guede.

Gamondi alisema mechi ilikuwa ngumu sana licha ya kutokea mambo mengi ndani ya uwanja ikiwamo kutopewa penalti pamoja na kutengeneza nafasi nyingi kwa kushindwa kuzitumia, lakini wachezaji walipambana na kufanikiwa kupata bao hilo la ushindi.

"Tulicheza mpira mzuri, nimefurahi wachezaji walitulia na kufanikiwa kukusanya pointi kwa bao pekee la Guede, mchezaji mzuri na mshambuliaji wa mwisho amefanya kazi nzuri.

"Kuhusu Bacca (Ibrahim), si majeruhi bali nimefanya mabadiliko ya safu ya ulinzi kwa kumpumzisha kwa sababu ya kucheza mechi nyingi na mfululizo kulingana na jinsi ya ratiba ya ligi ilivyo kwa sasa," alisema Gamondi.

Alieleza kuwa wako kwenye nafasi nzuri ya kutwaa taji la ubingwa, lakini bado hawajakuwa na asilimia 100 kwa hilo kwa sababu bado wana michezo mkononi na ligi haijaisha, hivyo wanatakiwa kuwa makini kusaka ushindi bila kuangalia waliopo chini yao wanafanya nini.

Kocha Mkuu wa Coasta Union, David Ouma, alisema wachezaji wake wamecheza vizuri licha ya Yanga kuwa na wachezaji wazoefu ambao waisaidia kufanikisha ushindi huo.

Alisema Yanga wamepata pointi tatu wakiwa pungufu baada ya mchezaji wake (Lawi)

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >